# Nipashe

Jumatano Desemba 9, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580424

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




Taifa laendelea 'kukalia' uchumi wa bahari kuu

Ukurasa 13

siasa

JUMATANO DESEMBA 9, 2020 HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 14

Kilichomvusha Mwalimu Nyerere kung'arisha nchi ndani ya miaka 10 uhuru wa Tanzania

MIAKA 59 YA UHURU

Namna Mwalimu Nyerere, Kawawa walikutana wakadumu 'damu damu'

• Kabla na baada uhuru, hadi wastaafu

Na Peter Orwa

KATIKA siku zilizopita waliohuhudia zama za uongozi wao, wajihi wa uhusiano wa Mwalimu Julius Nyerere na Rashid Kawawa, ulibeba sura ya kindugu, hata katika mwonekano mbele ya umma.

Iko wazi, Rais Nyerere alimtumia sana Waziri Mkuu Kawawa hasa katika katika zama za uongozi wake wa uwaziri mkuu na baadaye sana, Katibu Mkuu wa chama - CCM kufanikisha ajenda za kitaifa.

Kawawa alidumu kuwa 'jembe na mwadilifu wa Nyerere' aliyejulikana kitaifa katika utekelezaji kuanzia itikadi hadi 'hapa kazi,'hata kuna wakati alipokuwa katika nafasi nyinginezo za uwaziri, akiwamo asiye na wizara maalum.

Ulikuwa ufanyaji kazi wa timu halisi na hata watoto ngazi ya shule wakati huo siasa ya chama kimoja, kuna ushuhuda wa mengi hata katika mazuri ya kujifananisha katika staili yao michezoni "Mimi Nyerere na wewe Kawawa."

Ikumbukwe ni zama ambazo mfumo wa chama kimoja ulikuwa juu na itikadi ya nchi, Ujamaa na Kujitegemea, ulijenga kasi, wakubwa kwa watoto waliofautilia kuanzia shule hadi redioni walifahamu vyema na baadhi wakiwa katika matamshi duni ya kujifunza '...kujimetegea.'

Mwanzo wa watu hao kukutana na hata 'wakaiva' kiutendaji mzizi wake uko wapi? Ni aina ya majibu yaliyochukua muda kutafutwa, hadi katika zama ambazo wote hawakuwa madarakani na mengine zaidi ya hayo.

Wakati mfumo wa vyama vingi vinaanza tena mwaka 1992 baada ya kutoweka mwaka 1964. Mwalimu

Rais Julius Nyerere na Rashid Kawawa, katika zama za mwan-

pale aliposhindwa kukubali alichokitafsiri ni namna ya kejeli kutoka kwa aliyekuwa kiongozi wa nchi katika miaka 10 ya mwanzo wa uhuru.

Nyerere alitamka "angeniambia mimi tu nisingemjali sana, lakini kamkashifu Rashidi (Kawawa)... sitakubali, nitamshitaki!"Ilikuwa kauli nzito na iliyoonyesha thamani ya Kawawa na hata sura ya upendo wenye undugu wa kihistoria.

Msingi wa tamko hilo unaweza kuuganishwa na ushuhuda wa mwaka 2006 wilayani Tunduru, wakazi wake walipompokea Mzee Kawawa katika Uwanja Mdogo wa Ndege wa Misheni ya Mbesa, kwa ajili ya kuzindua kampeni za uchaguzi mdogo.

Kawawa alipokaribishwa katika chumba cha wageni, walimuimbia wimbo mkongwe "...eeh eeh TANU yajenga nchi..." ambao ulitawala sana katika zama za mwanzo za uongozi wa Mwalimu Nyerere, Ujamaa 'ukiwa mbichi.'

Badala ya kuungana nao walau kwa kutikisa kichwa au tabasamu, Kawawa alishindwa kujizuia kwa kutokwa machozi, hali iliyowafanya waimbaji kukatisha na wengi katika hadhira, fikra zilienda mbali kwa mtazamo "amekumbushwa mbali kwa kina Nyerere."

Aliyekuwa Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam marehemu, Kapteni mstaafu John Barongo, aliwahi kutoa

alipotaka historia ya wakongwe wa nchi zikawekwa sawa kabla hawajaondoka, kazi aliyofanya kwa mdomo na alirudia kwa andiko gazetini.

Naam! Niliamua kulichukulia kwa uzito stahiki, kuunganisha na kama hicho kilichowahi kunivutia miaka mingi redioni kutoka kwa aliyekuwa mwanataaluma wa historia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu Huria (OUT), Profesa Joseph Mbwiliza.

Mtaaluma huyo aliyewahi kukalia wadhifa naibu waziri kwa tiketi ya ubunge Kasulu na wakati fulani Mkuu wa Chuo cha CCM Kivukoni, alihimiza maboresho ya historia taifa, ulivyokuwa mkakati wa UDSM kutaka kutafiti wa kuweka sawa historia ya jamii ya Hadimu, visiwani Zanzibar.

Kimsingi, inaangukia kundi lile lile la wazo la Kapteni mstaafu Barongo. Hapo ndipo nami nikajiwekea ajenda ya kujua historia kufahamu siri ya muugano wenye ufanisi kiongozi, kati ya Mwalimu Nyerere na Mzee Kawawa.

MZIZI WA UHUSIANO

Wazungu wana usemi 'getting from the horse's mouth' kwa maana ya uhalisia unatoka kwa mhusika. Ni utekelezaji uliofanyikia muda mfupi baada ya kifo cha Mwalimu Nyerere, wakati kila pande wakidodosa kihistoria.

Mwanzo wa kazi hiyo ilikuwa faragha ya saa tatu na Mzee Kawawa nyumbani kwake Madale, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam na nyingine kama hiyo kwenye tukio la kumbukumbu la mwaka tofauti, nili-

UKURASA 11

**KOREA** yaimwagia Tanzania mkopo nafuu bil. 685/-

UKURASA 5




**KESI** ya mauaji ya Mawazo CHADEMA yaanza kunguruma

UKURASA 4

# Maalim Seif: Halikuwa jambo rahisi kukubali

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Maalim Seif Sharif Hamad kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Spika asema haoni sababu ya kufukuza wabunge CHADEMA

UKURASA 2

## DPP: Niko tayari kujiuzulu ikithibitika

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA SASA YAGEUZIA 'PIRA BIRIANI' LIGI KUU** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Maalim Seif: Haikuwa rahisi kukubali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema haikuwa rahisi kukubali nafasi hiyo, huku akieleza sababu za ACT-Wazalendo kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) kikatiba.

Akizungumza baada ya kuapishwa Ikulu ya Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alisema haikuwa rahisi kukubali kutokana na mambo yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Alisema vikao vya chama hicho pamoja na viongozi wake walikuwa na wakati mgumu na kwamba uamuzi huo uliwafikirisha mpaka kukubali kuingia katika serikali, Bunge na Baraza la Wawakilishi.

"Moja ya sababu zilizotufanya kufikia uamuzi huo ni imani yetu kwako binafsi, maneno yako, vitendo na ishara zako kuwa una nia njema na dhamira safi za kututoa tulikokuwa na kuibadilisha Zanzibar yetu katika nyanja zote," alisema.

"Tumeona wewe ni mtu tunayeweza kufanya kazi nawe, tunayeweza kusikilizana na tunayeweza kukupa nafasi uthibitishe nia yako njema. Nia yako ndiyo iliyotufanya na sisi tutangulize nchi kwanza, licha ya madhila yote yaliyojitokeza katika uchaguzi uliopita," aliongoza.

**NILIKATAA**

"Wenzangu walipokuja na wazo hili la sisi kuungana na wewe na baada ya kushauriana na wanachama wetu, niliwashauri kuwa sasa ni wakati wangu mimi kupumzika na kupeleka jina la damu mpya. Hawakunikubalia," alidokeza.

"Waliniambia, wewe ndiye uliyeongoza maridhiano na Rais Amani Karume mwaka 2009 na wewe ndiye uliyeshiriki Serikali ya Kwanza ya Umoja wa Kitaifa na Mheshimiwa Rais wa wakati huo, Dk. Mohamed Ali Shein. Wakaniambia maadam wewe ndio umelianza, basi ulimalizie," alisema.

"Wakasema wewe mtu mzima na utu uzima dawa. Wakanitaka nikubali ili nije kusaidia azma hii ya kutibu majeraha ya Zanzibar na kuyastawisha maridhiano. Sikuwakatalia ndio maana leo (jana) niko hapa.

"Hujikuta niko katika wakati mgumu kila ninapoona imani waliyonayo wananchi, ninaishiwa nguvu ila imani yao huongezeka na kunipa nguvu, imani yao ni wito mtakatifu unaonipa kuendelea kuwatumikia," alisema.

Maalim Seif alisema SUK iliyoasisiwa na Katiba ya Zanzibar kupitia marekebisho ya 10 ya Katiba ya mwaka 2010 ilikusudiwa kuwa chombo cha kusimamia, kuratibu na kuongoza juhudi za Wazanzibari kufikia maridhiano na Umoja wa Kitaifa.

**MSINGI WA SUK**

"Haikuwa na bado si lengo la Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuwa chombo cha kugawana vyeo kwa kambi za kisiasa. Ni vyema jambo hili tukalikumbuka kila wakati," alisisitiza:

Aidha, alisema SUK ni sawa na chombo cha usafiri na kwamba kwa msafiri yeyote awe wa baharini, angani au nchi kavu, lengo lake sio kuingia katika meli, ndege au gari, huku lengo lake ni kufika safari aliyopanga ya Wazanzibari ni maridhiano ya kweli, mshikamano na umoja wa kitaifa.

Kwa mujibu wa Maaalim Seif, maridhiano yale yalilenga siyo tu kuwa na mfumo shirikishi katika uendeshaji wa nchi, bali yalikusudia kuondoa kabisa siasa za mivutano zilizotawaliwa na chuki, uhasama na visasi ambavyo kwa njia moja au nyingine vimekwamisha ustawi wa nchi yetu kwa muda mrefu sana.

"Kwa masikitiko makubwa sana, maridhiano yale yalikwama njiani. Kwa sababu hii basi uchaguzi wa mwaka 2020 umeturejesha tulikotoka. Uchaguzi umetuachia na uhasama mkubwa zaidi, umetuachia na maafa makubwa zaidi," alisema na kuongeza:

"Haya ni mambo ya aibu sana na fedheha kwa nchi yetu. Hili ni doa katika historia ya nchi yetu na hatuna budi kuchukua hatua thabiti za kulifuta doa hili kwa njia itakayowaridhisha waathirika na wananchi kwa ujumla. Kuja kwetu serikalini na kuingia kule barazani, ni ishara ya nia yetu njema ya kutaka kushirikiana na wewe kutafuta majawabu ya kudumu ya matatizo haya."

"Leo si siku ya kusema sana. Bila shaka tutapata wasaa mwingi wa kukaa pamoja, kushauriana na kutafakari mustakhabali wa Zanzibar yetu na nini kwa pamoja tunaweza kufanya. Nikuhakikishie juu ya dhamira yetu safi mimi na wenzangu ya kufanya kazi na wewe kwa manufaa ya Wazanzibari wote," alisema.

**MWINYI APONGEZA**

Akizungumza baada ya kumwapisha kiongozi huyo, Dk. Mwinyi alimpongeza Maalim Seif na chama chake kwa kukubali uteuzi huo na kwamba kupendekezwa kwa jina lake na kuteuliwa ni ushahidi na imani ambayo wanachama na viongozi wa chama chake wamewekeza juu yake.

"Nami kwa kuheshimu na kutambua uzito wa imani hiyo kwake, na imani yangu kwake, nikamteua bila kigugumizi chochote kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Mimi ni muumini wa umoja wa kitaifa, mshikamano, udugu na maridhiano. Naamini kwa dhati ya moyo wangu kuwa maridhiano ni njia nzuri ya kujenga umoja wa kijamii na ustawi wa nchi na wananchi wake.

"Ni jambo linalowaleta watu pamoja, linaloileta nchi pamoja, linalotuhakikishia amani na mshikamano wa kudumu. Kizazi cha leo cha Wazanzibari ambao asilimia 93 wamezaliwa baada ya Mapinduzi na Muungano, kinayo dhima ya kipekee ya kufunga ukurasa wa uhasama na chuki, na kufungua ukurasa mpya wa upendo na maridhiano.

Matamanio yangu, bila shaka na ya wengi wanayoitakia mema Zanzibar yetu, ni kuondoshwa kwa majeraha na madonda ya historia yetu ya Zanzibar, ambayo yameendelea kuwa mtihani kwetu mara kwa mara katika chaguzi zetu," alisema.

Dk. Mwinyi aliahidi kushauriana na Maalim Seif kujaza nafasi zilizobaki katika Baraza la Mawaziri na namna bora ya kuendesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa.


**UBALOZI WA DENMARK, AMERIKA DSM FINLAND NA UINGEREZA DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Denmark, Amerika, Finland na Uingereza watauza kwa mnada wa hadhara Magari, Pikipiki, Magenereta & Fanicha za nyumbani / ofisi tarehe 12 December, 2020 Jumamosi saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fenicha na Appliances zitaanza kuuzwa saa 4:00 asubuhi:** Sofa sets, Sofa Bed, China Base, Hutch, Chest drawers, Dresser, Vitanda ,Magodoro , Coffee table, Book case, Dining Table, Viti, Meza za ofisi, Viti, Fridge, Freezer, Freezer za Biashara, TV, Majiko ya umeme, Washer, Dryer, A/c Split unit,na vingine vingi.

**Magari , Pikipiki na Majenereta Yataanza kuuzwa saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Rav4 Saloon | ZCA 26 Petrol Engine | 2000 | Bado |
| 1 | Ford FIGO Sloon | 4 Cylinder Petrol Engine | 2012 | Bado |
| 1 | Land Rover Station Wagon | Freelander 2 Petrol Engine | 2012 | Bado |
| 1 | Honda Motorcycle | XL 125 Petrol | 2010 | Bado |
| 3 | Generators silence 33KVA | Perkins Engine Diesel | - | Bado |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street tarehe 10 mpaka 11 December, 2020 kuanzia saa 4:00. asubuhi mpaka saa 10:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi wa fanicha atatakiwa kulipa malipo yote pale pale. Na mnunuzi wa Gari au Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 18 December, 2020 saa 10:00 jioni, ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Generator litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa .
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB bank yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama yalivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali zote zitakazouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**NKRUMAH STREET MKABALA NA CO-CABS**
**SIMU NA: 0754-284 926, 0767 284 926**
**Email : universalauction@hotamail.com**
**DAR ES SALAAM.**


# Spika Ndugai asema haoni sababu ya kufukuza wabunge CHADEMA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, (pichani) amesema atakuwa wa ajabu endapo akiwafukuza wabunge wa viti maalum 19 kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kosa la kuwaapisha. Ndugai aliyasema hayo jana, alipokuwa akiwaapisha wabunge wawili walioteuliwa na Rais John Magufuli hivi karibuni Dk. Dorothy Gwajima na Mhandisi Leonard Chamuriho, ambao wameteuliwa kuwa mawaziri wa Afya na Ujenzi.

Alisema Watanzania waendelee kuvumilia na kuangalia sinema inayoendelea ambayo haijawahi kutokea kwenye nchi yoyote duniani.

Alisema: "Kwamba Spika unaambiwa uwafukuze wabunge 19 wanawake halafu unauliza kosa lao nini, unaambiwa kosa lao ni kwa sababu waliitikia wito wako wa kuja kwako halafu na wewe ukawaapisha." "Hivi duniani kote mmewahi kuona wapi kitu kama hicho? Kwa sababu kwa njia ya wale na wanaofanana nao wa viti maalum 'route' yao kwa Spika ina route mbili, njia moja ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuniandikia na kusema hawa wanastahili kuwa wabunge mheshimiwa Spika waapishe, na huo ndio utaratibu ulifuatwa," alisema.

Aliongeza: "Njia ya pili ni kwamba wanaoapishwa kwa njia hiyo huwa majina yao yanatangazwa kwenye Gazeti la Serikali, na walishatangazwa kwa kuorodheshwa kwa majina." Alisema kuwa hayo yametekelezwa ipasavyo na Spika amewaapisha. "Halafu mtu anasema kosa la hao ni wewe kuwaita na kuwaapisha kwa hiyo wafukuze hivi na mimi si nitaingia kwenye 'guiness book'. Spika wa ajabu kabisa ambaye hajawahi kutokea duniani kwa kosa la kuwaapisha."

Spika Ndugai alisema: "Siku hizi Watanzania wanapenda tamthilia na hii nayo ni tamthilia kama jambo hili lina ulakini mahali ufuatiliaji wake sio kwa Spika, nalo lina route mbili au zaidi, kwanza kufuatilia NEC maana wao wanaratibu na kuniletea majina."

Alisema majina yote yaliyoletwa na NEC tayari yamefanyiwa kazi na kwa upande huo hakuna shida.

"Route ya pili kama jamaa zetu wanasahau ni mahakamani na ndio inaweza kuniambia Mheshimiwa Spika, kuna walakini kwa mbunge chukua hatua hii, hakuna route nyingine kwa kosa hilo labda kama kosa jingine, kosa kwamba kwanini wameapishwa, kwani wewe ulitakaje?"

Alisema. Ndugai alisema tamthilia ziachwe kwao ziendelee na kwamba njia hizo mbili zinasaidia kutatua migogoro yao. "Wabunge mlioapishwa endeleeni na shughuli zenu za kibunge popote mlipo na sisi tunaendelea kuna ukarabati mkubwa tunafanya, vitendea kazi tumeshawapa, Februari tukifika hapa tutaanza na mjadala wa wiki moja wa hotuba ya Rais, pia kutakuwa na mjadala wiki ya pili wa mipango ya serikali ambayo itasaidia kutengeneza bajeti ya mwaka 2021/22," alisema.

HABARI KITAIFA

# DPP asema yuko tayari kujiuzulu

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKURUGENZI wa Mashtaka Nchini (DPP), Biswalo Mganga, amesema yuko tayari kujiuzulu kama Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kitapeleka hoja za msingi na akazipima kuhusu sakata la kada wa chama hicho, Nasrat Hanje, aliyetolewa gerezani na kuapishwa kuwa mbunge wa viti maalum.

Alikuwa akijibu hoja ya watu wanaohoji kufanyakazi kisiasa na kutakiwa kujiuzulu, alipokuwa katika mahojiano kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na ITV, kila Jumatatu.

"Kujiuzulu kuna taratibu zake, maana yake ukisema tu mtu amesema ajiuzulu ni sawa sawa na kusema nimeshindwa kufanya majukumu yangu ya kikatiba, kama kuna sababu wanazoweza kuleta nikaziona nikazipima niko tayari," alisema Mganga.

Alisema katika suala la kada wa chama hicho (Nasrat) ambalo amefanya maamuzi magumu ambayo pengine CHADEMA hawajayapenda, haoni kuwa sababu ya mtu kujiuzulu.

"Anayeweza kujiuzulu kwa namna hiyo si kwamba amejiuzulu kwa sababu ya hayo mashinikizo basi yeye mwenyewe anakuwa ameshindwa kutimiza majukumu yake," alisema.

Mganga alisema Watanzania wafahamu kwamba DPP siyo mwanasiasa, hafanyi kazi kisiasa na katika kudhihirisha hilo katika shughuli zake wapo wanachama wa CCM, CHADEMA, CUF na vyama vingine ambavyo amewafungulia mashtaka.

Alisisitiza kuwa kama angekuwa anafanya kazi kisiasa wengine asingewafungulia mashtaka.

"Kwa mfano kwenye kampeni za uchaguzi huu ulioisha, Tarime kuna viongozi fulani wa CCM walifanya makosa wakafanya vurugu, wakamuua mtu wakiwa kwenye kampeni na ilikuwa siku ya mwisho, nilichosema si wamefanya kosa wawekwe ndani na tunavyoongea bado wapo ndani," alisema.

Alisema katika matukio anachojali ni ushahidi na amefanya hivyo wakati wa kutekeleza majukumu bila kuangalia chama kwasababu Katiba yenyewe inamtaka afanye kazi bila upendeleo.

Aliwahakikishia Watanzania kwamba yaliyofanyika kwenye mchakato wa kada huyo wa CHADEMA yamefanyika kwa mujibu wa Katiba na taratibu za sheria ya nchi.

"Ukiangalia kwenye Katiba ibara ya 59, ibara kubwa 'b' 54, imeweka wazi wakati DPP anatekeleza yote hatakiwi kuingiliwa na mtu yeyote au chombo chochote, hata chama cha siasa ni chombo," alisema.

Mganga alisema chama chochote kinachojaribu kuweka shinikizo kwa DPP afanye maamuzi kwa kadri wanavyotaka wao wanakuwa wanavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kiongozi yeyote yule anayemuwekea DPP mashinikizo afanye uamuzi kwa kadri anavyotaka, anakuwa anavunja Katiba, mimi nimeapa kuisimamia Katiba na sheria zilizopo na hivyo lazima niishi kwenye kiapo," alisema.

Pia, alisema suala la kuwafutia watu kesi lipo kwenye Katiba ibara ya 59 'B' ibara ndogo ya pili ambayo mojawapo ni kufungua mashataka na kuyaendesha na DPP anafuta kesi kuzuia matumizi mabaya ya utoaji haki.

Akizungumzia vigezo vilivyotumika kumfutia kesi kada wa CHADEMA, alisema yeye (Nasrat) na wenzake walipokuwa Singida kwa makusudi na kwa kunajisi wimbo wa taifa na bendera ya taifa, waliamua kuingia kwenye kikao chao wakaimba wimbo wa taifa na kupandisha bendera ya CHADEMA halafu wakaongeza maneno 'Mungu ibariki CHADEMA'.

Alisema tafsiri yake ni mbaya zaidi tofauti na watu wanavyofikiria. "Kwanza maana yake hautambui mamlaka iliyopo nchini kama kwamba unataka kupindua nchi ndo maana unapandisha bendera yako, umetengeneza wimbo wako wa taifa lako tofauti na ule ambao unatambulika."

Alisema baada ya kuona hivyo, aliamua kuwafungulia mashtaka watuhumiwa na wakaenda gerezani kwasababu kilikuwa kipindi cha kuingia kwenye uchaguzi. "Kama watu wanataka kuanza taratibu za kuanzisha taifa lao, wimbo wao wa taifa wanaoujua tofauti na wimbo wa taifa unaojulikana sasa, hawa lazima tushughulike nao."

Alisema watuhumiwa hao wakiwa gerezani kukatokea viongozi wakuu wa CHADEMA walipokuwa wanafanya mkutano wao wa kuchagua viongozi mkutano wa Kamati Kuu ya chama hicho wakafanya kitendo kama hicho.

"Mimi DPP, na kwa kuangalia Katiba nikasema lazima tuangalie maslahi ya nchi, nikasema haitakuwa na afya kuwafungulia wote hao mashtaka na walifanya kwa sababu walikuwa wanajua wenzao walishafunguliwa mashtaka na wako gerezani," alisema.

Alisema viongozi wa Kamati Kuu walijua wakifanya hivyo, DPP atawafungulia mashtaka kama alivyowafungulia wa Singida halafu wananchi na makundi yanayowasapoti wataleta vurugu ionekane kwamba Tanzania hakuna amani na hakuna uchaguzi huru.

"Katika kusimamia sheria lazima utumie busara, ndiyo hayo maslahi ya taifa, hivyo katika kulinganisha maslahi ya taifa nikasema haitakuwa na afya zaidi kuwapeleka mahakamani kwa kipindi hicho ngoja waendelee na kampeni waingie kwenye mchakato wa uchaguzi uendelee kama kawaida wakati natafakari niwapele au ni waachie," alisema.

Alisema haitakiwi kufanya uamuzi kwa upendeleo wa makusudi na aliona kwa sababu makada wengine wamefanya kosa lilelile, wale waliofanya kosa Singida wafutiwe mashtaka.

"Hata ambaye anasema aliachiwa usiku inawezekana hakuwapo, muda wa kuachia upo kwenye hati ya mahakama ya kumuachia. Kama kuna mtu anaweza akaja na ushahidi kwangu kwamba siku hiyo usiku hakimu alikuwapo gerezani ndio akamuachia, ailete, lakini mimi najua hati hiyo ilisajiliwa mahakama ya Singida muda ambao mahakama ilikuwa inafanya kazi, hiyo ilikuwa ni 'process' (mchakato) ambayo ilikuwa inaishia tu," alisema.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

Miaka 59 ya Uhuru wa Tanganyika

9 DESEMBA, 2020



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli** pamoja na watanzania wote katika kuadhimisha **miaka 59 ya Uhuru wa Tanganyika.**

tratanzania 0744-233 333 www.tra.go.tz

# Kesi ya mauaji ya Mawazo wa CHADEMA yaanza kunguruma

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, imeanza kusikiliza kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Geita, Alphone Mawazo, inayowakabili washtakiwa watano.

Katika kikao cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Geita chenye mamlaka ya nyongeza kutoka Makao Makuu Mwanza, shauri la mauaji namba 9/2019.

Washtakiwa hao ni Alfan Apolinari (41), Epafula Zacharia (39), Hashimu Sharifu (45), Habibu Feruzi (34) na Kululinda Bwire (31), wote ni wakazi wa Katoro mkoani Geita.

Washtakiwa walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita jana, majira ya saa 3 asubuhi na kupandishwa kizimbani majira ya saa 7:30 mchana mbele ya Naibu Msajili Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza ambaye ni Hakimu Mkazi Mwandamizi Mwenye Mamlaka ya Ziada (Extended Jurisdiction), Frank Mahimbali na waliposomewa shtaka lao la mauaji.

Hata hivyo, walikana na kurejeshwa rumande kutokana na kosa la mauaji kutokuwa na dhamana. Upande wa Jamhuri ukiongozwa na mawakili watatu Javelin Rugaihuruza ambaye ni Wakili wa Serikali Mkuu, Hezron Mwasimba, Wakili wa Serikali Mwandamizi na James Pallangyo walidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, na kuwa wako tayari kwa ajili ya mahakama kuanza kumsikiliza shahidi mmoja.

Upande wa utetezi unaongozwa na mawakili wa kujitengemea watano ambao kila mmoja anamtetea mshtakiwa mmoja mmoja ni Yisambi Siwale, Flora Enosy, Laurent Bugoti, Abel Sizya na Paul Hombo.

Hakimu Mahimbali alikubaliana na ombi hilo na shahidi mmoja wa upande wa Jamhuri alitoa ushahidi.

Shahidi huyo Mkuu wa Upelelezi katika Kituo cha Polisi Katoro ambaye kwa sasa ni mkazi wa Bihalamulo Mkoa wa Kagera, Mashaka Mahira (56), akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Rugaihuruza, alidai kuwa majukumu yake yalikuwa kulinda amani pamoja na kukamata watuhumiwa na kuwahoji kisha kuwafikisha mahakamani.

Alidai kuwa Novemba 14, mwaka 2015, majira ya mchana alikuwa kazini na muda huo alikuwa anakunywa chai kwenye mgahawa ndipo akapigiwa simu akitakiwa kwenda kituoni.

Alidai wakati anatoka mgahawani alimwona mtu mrefu mweupe ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Geita akiongea na simu na alikuwa na wasiwasi, na kuwa alipomkaribia, aliamua kuondoka eneo hilo.

"Baada ya hapo niliingia kituoni ambapo niliwakuta WP Stella na WP Gresi na kulikuwa na watu wengine wateja wawili walivaa koti jeusi na suruali nyeusi na mwingine alikuwa amevaa suruali nyeusi na shati jeupe ambaye alimjua kwa jina la Alois Bayona akiwa amevimba mdomo na alipowauliza wamepingwa na nani walimjibu kuwa wamepigiwa eneo la CCM Rudete na kuwa wamepigwa na watu wasiowafahamu.

Shahidi huyo alidai, alitoa maelekezo watu hao waandike maelezo yao, na kuwa mmoja aliyeumia apewe PF3 ili akapate matibabu.

Alidai zaidi baada ya maelekezo hayo aliona gari aina ya Hiace yenye namba za usajili T 216 CLQ ambayo ilikuwa ikiendeshwa na Lucas ambaye alidai kuna mtu ameumia, hivyo wanaomba msaada.

## Mwalimu mkuu na mwenyekiti kortini kwa madai ya rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MWALIMU Mkuu wa Shule Msingi Isabilo na Mwenyekiti wa Kijiji cha Isabilo, wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Geita kwa tuhuma za rushwa.

Wanatuhumiwa kushawishi hongo ya Sh. 400,000 kutoka kwa Mariana Lelemba ili kumwachia kijana wake, Patrick Lelemba, aliyekuwa amekamatwa kwa madai ya kumtorosha mwanafunzi (jina linahifadhiwa). Washtakiwa hao, Joseph Mpanduji (36) ambaye ni Mwalimu Mkuu na Linus Mtabe (58), Mwenyekiti wa Kijiji cha Isabilo wanadaiwa wametenda jambo hilo kunyume cha kifungu cha 15 (a) (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 iliyorekebishwa ya mwaka 2019. Mpanduji na Mtabe, walifikishwa jana mahakamani majira ya saa 3:00 asubuhi na kupandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Sosthenes Kiiza. Waliposomewa shtaka hilo walikana na wako nje kwa dhamana wa mdhamini mmoja mmoja ambao waliwasilisha barua ya utambulisho kutoka kwa mwajiri wao na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. 500,000 kwa kila mdhamini.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, uldai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

Hakimu Kiiza alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Januari 7, mwakani.

Akisoma hati ya mashtaka, Murusuri alidai kuwa Novemba 7, mwaka huu, katika kijiji cha Isabilo mkoani Geita, washtakiwa kwa pamoja walimkamata Lelemba na kumweka mahabusu kwa madai ya kumtorosha mwanafunzi wa Shule ya Msingi Isabilo.

Kutokana na tuhuma hizo, walidai hongo ya Sh. 400,000 ili wasimchukulie hatua za kisheria kwa kumtorosha mwanafunzi huyo. Wakili huyo aliendelea kudai kuwa Lelemba aliwasiliana na mzazi wake ili kufanikisha kupatikana kwa fedha hizo na mzazi wa Patrick alitoa taarifa TAKUKURU na hatua stahiki zikachukuliwa na kuwakamata kisha kuwafikisha mahakamani.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MKUU WA MKOA ARUSHA
59 Miaka ya Uhuru



Mkuu wa Mkoa, Watumishi na Wananchi wote wa Mkoa wa Arusha Tunaungana na Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na Watanzania wote katika kuadhimisha Miaka 59 ya Uhuru.

MAWASILIANO
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha
Postal Address: 3050 Arusha,
Telephone: 27 254 5608
Mobile: 027 254 4950,
Email: ras@arusha.go.tz

**HABARI KITAIFA**

# Korea yaipa Tanzania mkopo nafuu bil. 685/-

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI ya Tanzania imesaini mkataba wa mkopo wa masharti nafuu kutoka Korea Kusini wenye thamani ya Sh. bilioni 684.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa vituo viwili vya kupozea umeme.

Akizungumza jana baada ya kusaini mkataba huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema mkopo huo umetolewa na Korea kupitia Mfuko wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EDCF).

Aidha, alisema mkopo huo ni kwa ajili ya ujenzi wa vituo viwili vya kupozea umeme katika njia ya kusafirishia umeme ya Kigoma - Nyakanazi gridi ya Taifa Kaskazini Magharibi ambapo umepata Sh. bilioni 102.9.

Kadhalika, alisema fedha hizo zitasaidia bajeti kuu ya serikali kiasi cha Sh. bilioni 91.4 na mradi wa uboreshaji wa huduma za maji katika Jiji la Dodoma utapata Sh. bilioni 160.

"Fedha hizi zitasaidia mradi wa kuimarisha miundombinu ya upimaji ramani Sh. bilioni 148.6 na ujenzi wa daraja la Salender utapata Sh. bilioni 74.5," alisema.

Alisema mkopo huo utachangia maendeleo na kuleta mageuzi ya kiuchumi, na kwamba mradi wa umeme utatoa umeme wa uhakika mikoa ya Kaskazini Magharibi ya nchi na kupunguza gharama za uendeshaji na ukarabati wa mitambo ya uzalishaji.

Alisema lengo la serikali ni kubadilisha mitambo inayozalisha umeme kwa njia ya mafuta ya dizeli na kuingiza mikoa hiyo kwenye gridi ya taifa pia itasaidia kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa.

Kuhusu uboreshaji wa mtandao wa maji taka Jiji la Dodoma, alisema mradi utalenga kuboresha mradi wa majitaka kwa kujenga mtambo wa kutibu majitaka hayo na kupanua wigo wa mabomba ili kupunguza uchafuzi wa mazingira chini na juu ya ardhi.

Balozi wa Jamhuri ya Korea Kusini, Cho Tae Ick, alisema hata nchi yao imeendelea kiuchumi kutokana na mikopo yenye masharti nafuu.

Balozi Ick aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kusimamia mapato yake, ambayo yamewezesha kuingia kwenye uchumi wa kati.

# TANESCO yajitosa uchunguzi moto shuleni

**Na Richard Makore,** MWANZA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Mwanza, limesema limeanza kufanya uchunguzi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama kwa shule na vyuo ili kuangalia mfumo wa umeme kubaini chanzo cha baadhi ya majengo kuungua moto mara kwa mara.

Sambamba na hilo, shirika hilo linatarajia kuanza kutumia nguzo za zege kusambaza umeme badala ya za miti ambazo zinatumika kwa sasa. Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana jijini Mwanza, Meneja wa TANESCO Kanda ya Ziwa, Henryfried Byabato, alisema uchunguzi wa mfumo wa umeme una lengo la kubaini chanzo cha kuungua majengo hayo.

Byabato alisema, timu maalumu inayoshirikisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), TANESCO na wataalam wengine, wameanza kazi hiyo katika Kanda ya Ziwa.

Katika miaka ya karibuni, kumekuwa na matukio ya majengo ya shule mbalimbali kuungua moto na kuteketeza mali za wanafunzi huku chanzo kikidaiwa kuwa ni hitilafu ya umeme inayosababishwa na mfumo mbovu wa umeme.

Kuhusu watu wanaotaka kufungua viwanda mbalimbali mkoani Mwanza, Byabato alisema kuna megawati 132 za umeme ambazo zinatosha kuwahudumia.

Alisema mpaka sasa matumizi ya mkoa mzima ni megawati 59 pekee na kwamba bado wana zaida ya kutosha ya nishati hiyo.

Katika hatua nyingine, alisema TANESCO imeanza kutengeneza nguzo za umeme ambazo zitasaidia kupunguza gharama za matengenezo kwa kuwa zinadumu kwa miaka 50.

# Vyakula vyashusha mfumuko wa bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imesema mfumuko wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia Novemba, 2020 umepungua hadi asilimia 3.0 kutoka asilimia 3.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba, 2020.

Kupungua kwa mfumuko huo kumechangiwa na kupungua kwa bei ya baadhi ya bidhaa za vyakula ikiwamo mchele na mahindi. Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii wa Ofisi hiyo, Ruth Minja, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya mfumuko wa bei.

Alitaja baadhi ya bidhaa za vyakula zilizopunguza bei kwa Novemba 2020 ikilinganishwa na Novemba 2019 ni mchele kwa asilimia 4.5, mahindi kwa asilimia 14.3, unga wa mahindi kwa asilimia 5.7.

"Unga wa mtama kwa asilimia 4.4, viazi vitamu kwa asilimia 2.6, vyakula vya watoto kwa asilimia 1.8 na ndizi za kupika kwa asilimia 4.9," alisema.

Minja alisema mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa Novemba 2020 umepungua hadi asilimia 2.8 kutoka asilimia 3.4 kwa mwaka ulioishia Oktoba, 2020.

Kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki, Mkurugenzi huyo alisema Kenya mfumuko kwa kipindi hicho umeongezeka hadi asilimia 5.46 kutoka asilimia 4.84 kwa Oktoba, 2020.

"Kwa Uganda, mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Novemba, 2020 umepungua hadi asilimia 3.7 kutoka asilimia 4.5 kwa mwaka ulioishia Oktoba, 2020," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC
TANZANIA SHIPPING AGENCIES CORPORATION

Maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa Tanzania



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli**

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), tunapenda kuungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na Watanzania wote katika kusherehekea maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa Tanzania.

**TASAC** tutaendelea kudhibiti na kusimamia huduma za bandari na usafiri wa meli, usalama, ulinzi wa vyombo vya usafiri majini na mazingira na kufanya biashara ya meli kwa matokeo chanya ya taifa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua muhimu kudhibiti bei kubwa mafuta ya kula

**JUZI** tuliandika habari ikionyesha kupanda kwa bei ya mafuta ya kula nchini kwa wastani wa Sh. 1,000 hadi 10,000, hivyo kilio kikubwa kwa watumiaji. Katika habari hiyo watumiaji wa hali ya chini walipaza sauti zao juu ya ongezeko hilo na namna linavyowakwamisha katika shughuli za ujasiriamali kama mamalishe, wakaanga chips, mihogo na samaki.

Mathalani, lita moja ya mafuta ya alizeti katika baadhi ya maeneo ilifika Sh. 5,000 kutoka 3,500, huku lita tano ikifika 30,000 kutoka 25,000.Kutokana na kupaa kwa bidhaa hiyo muhimu kwa maisha ya kila mmoja, waliiomba serikali kuingilia kati ili kutoa suluhisho la kudumu. Baadhi ya sababu zilizoelezwa kusababisha kupaa kwa bei ni mvua nyingi iliyopelekea wakulima kutokuvuna alizeti yao kwa wakati na kuipeleka mashine kwa ajili ya kukamua mafuta.

Kupitia vyombo vya habari vya serikali, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Ludovick Nduhiye, alikaririwa akisema kuwa serikali inafuatilia sababu za kupaa kwa bei ya mafuta.

Aidha, alisema ametoa maelekezo kwa wasaidizi wake wakiwamo maofisa wa Mamlato ya Mapato Tanzania (TRA), kupata taarifa za hali ya upatikanaji mafuta bandarini, takwimu za sasa za mafuta na hali ya ukamuaji wa mafuta ilivyo.

Pia, vyombo hivyo vilinukuu taarifa ya Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipa Kodi TRA, Richard Kayombo, kuwa wameshikilia meli mbili za mafuta ya kupikia na vielelezo vinaonyesha meli hiyo ni ya mafuta ghafi. Kwamba meli hizo zimekwama bandarini Dar es Salaam kutokana na mvutano wa kiwango cha tozo ya kodi inayodaiwa kusababishwa na TRA.

TRA ilifafanua kuwa meli hizo zimekwama bandarini kutokana na kutowasilisha vithibitisho kama mafuta hayo ghafi au yanatakiwa kulipiwa kadi ya asilimia 10 au yameshachakatwa na kutakiwa kulipia asilimia 25. Katika maeneo mbalimbali nchini bei ya mafuta ya nje ya nchi inalingana na bei ya mafuta yanayozalishwa ndani, jambo ambalo linazua maswali mengi.

NI muhimu sana kwa serikali kuchukua hatua za haraka kwa jambo hili kwa kuwa ni maumivu kwa mwananchi wa kawaida.


Mathalani, hivi karibuni bei ya saruji ilipaa kiasi cha mfuko kufika Sh. 30,000 kwa bidhaa inayozalishwa nchini, na siku chache mafuta yakapanda bei. Saruji haigusi mimilioni ya watu moja kwa moja kwa kuwa suala la ujenzi linaweza kusubiri, lakini kula chakula bila mfuta si suala la kusubiri, maana yake halina dharura.

Inapotokea mafuta yamepanda bei maana yake vyakula vitapanda bei na huenda watu wakaacha kununua vilivyopikwa na kuamua kupika wenyewe ili kumudu gharama za maisha. Mafuta yakipanda maana yake ni kuwaumiza mama lishe, wakaanga mihogo, chips, samaki na viazi ambao wanatafuta kipato kidogo kwa ajili ya kuwawezesha kuendelea kuishi.

Ni vyema hatua zichukuliwe ili kudhibiti kupanda bei kwa bidhaa hii muhimu kwa maisha ya Mtanzania pamoja na kudhibiti kupanda kwa saruji ambayo ni muhimu katika maendeleo ya makazi na miundombinu. Kunapotokea kupotea sokoni kwa bidhaa ndiyo sababu mojawapo ya kupanda kwa bidhaa husika, kwa kuwa wapo watakaotumia mwanya huo kujipatia fedha zaidi katika wakati huu wa soko huria. Katika nyakati hizi za soko huria, bei hupangwa na hali ya soko na serikali imeshajiondoa katika kupanga bei za bidhaa.Hata hivyo, inapotokea wananchi wameumia, serikali inawajibika kuingilia kati kuhakikisha inaweka mambo sawa kwa kutumia mifumo yake ili kumlinda mlaji na mfanyabiashara.

Tunarajia kuona matokeo mazuri ya kuendelea kumlinda mlaji na mfanyabiashara, kwa kuwa ni lazima wawepo ili walipe kodi za serikali ambazo ndiyo zitaendesha nchi, ikiwamo kutekeleza miradi ya maendeleo yenye manufaa kwa wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hongera kuishi miaka 59 kwa mshikamano, utulivu na upendo

Na Sabato Kasika

**TANZANIA** inasherehekea miaka 59 ya uhuru leo na kwa muda wote wananchi wameendelea kuishi kwa umoja, mshikamano, utulivu, upendo na amani kwa miongo yote bila kubaguana kwa hali yoyote.

Licha ya Tanzania kuwa na zaidi ya makabila 100, bado wanaendelea kuwa wamoja huku lugha kuu ya mawasiliano ikiwa ni Kiswahili, ambacho kinazungumzwa kote mijini na vijijini.

Watanzania hawana budi kusimama kidete kuilinda zaidi kwa manufaa ya kizazi kilichopo na vijavyo.

Inatia moyo kuona Tanzania inatimiza miaka 59, raia wake wakiendelea kuishi kwa mshikamano licha ya kuwapo makabila mengi, tofauti na baadhi ya nchi zenye makabila machache lakini zina migogoro ya ukabila na udini.

Kuwapo hali hiyo nchini, si kwamba inatokana na bahati bali ni juhudi za waasisi wa taifa za kuwaunganisha Watanzania na kuhakikisha wanakuwa wamoja bila kujali tofauti za makabila au dini.

> **Kuwapo hali hiyo nchini, si kwamba inatokana na bahati bali ni juhudi za waasisi wa taifa za kuwaunganisha Watanzania na kuhakikisha wanakuwa wamoja bila kujali tofauti za makabila au dini.**

Mwalimu Julius Nyerere ni miongoni mwa watu muhimu wa kukumbukwa katika jambo hilo ambalo linawafanya raia watembee kifua mbele bila hofu ndani ya nchi yao.

Wakati nchi inaadhimisha miaka 59 ya uhuru, ni vyema kukumbuka mchango wake ambao umemfanya aheshimike ndani na nje ya Tanzania kwa kuhimiza umoja wa kitaifa, utu, heshima na haki msingi za binadamu.

Aliijenga Tanzania yenye amani na kimbilio kwa nchi jirani ambazo zimekuwa zikikumbwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Hivyo miaka 59 ya uhuru iwakumbushe wazalendo kuendelee kujenga na kuimarisha imani.

Kwa ujumla ni kwamba, Watanzania waipende na wawe wazalendo kwa nchi yao dhidi ya maadui wa ndani na nje ya nchi yao, ili waendelee kufaidi matunda ya mama Tanzania.

Tangu serikali ya awamu ya kwanza hadi sasa inaamini kwamba amani, utulivu, umoja na mshikamano ni mambo ya msingi kwa Watanzania na yanahimizwa na wadau wakiwamo viongozi wa dini.

Kuendelea kuwapo amani kunaifanya Tanzania kuwa kimbilio la watu wanaotoka katika nchi zenye machafuko ya kisiasa kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za udini na ukabila.

Kwa kuwa Watanzania wanaunganishwa na Utanzania wao huku kila mmoja akiwa na kabila na dini yake, ni wajibu wa kila mmoja kuzingatia hilo na kuliendelea kwa manufaa ya kizazi hiki na kijacho.

Watu wenye nia ya kuvuruga umoja wa kitaifa, wasipewe nafasi, badala yake wajifunze kwa nchi zenye vita, kisha wachukue hatua za kulinda amani na utulivu, mshikamano na umoja uliopo.

Jambo la muhimu ni kila Mtanzania kutokubali kudanganywa na watu wasioutakia mema umoja uliopo ambao umeifanya Tanzania kutimiza miaka 59 huku wananchi wakiendelea kuishi kwa amani.

Ikumbukwe kuwa mwaka jana Tanzania ilitangaza kuongoza amani katika nchi za Afrika Mashariki, hiyo ikiwa ni kwa mujibu wa ripoti ya Global Peace Index (GPI) inayotolewa na taasisi ya uchumi na amani (IEP), yenye makao yake makuu mjini Sydney nchini Australia.

Tanzania ilishika nafasi ya saba kwa kuwa nchi yenye amani kwa mataifa ya Kusini mwa Jangwa la Sahara na duniani, ikiwa imeshuka kutoka nafasi ya 51 mwaka 2018 hadi nafasi ya 54 mwaka 2019 kati ya nchi 163.

Nchi za Iceland, New Zealand, Uholanzi, Austria, Denmark, Canada, Singapore, Slovenia, Japan, na Jamuhuri ya Czech zilizoorodheshwa kuwa na amani zaidi duniani.

Wakati Tanzania ikiongoza Afrika Mashariki, ni vyema kila mmoja aendelee kuimarisha amani kama njia ya kumuenzi Baba wa Taifa ambaye ni mwasisi wa mshikamano miongoni mwao.

HABARI KITAIFA

# JPM aongoza mamia kumuaga Jaji Nsekela

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amewaongoza viongozi na wakazi wa Dodoma kuaga mwili wa Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Harold Nsekela, aliyekuwa Kamishna wa Maadili ya Viongozi wa Umma.

Jaji Nsekela alifariki dunia Desemba 6, mwaka huu, jijini Dodoma baada ya kuugua kwa muda mfupi na anatarajiwa kuzikwa mkoani Mbeya kesho.

Tukio hilo lilifanyika jana katika viwanja vya Chinangali Park na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu (pichani).

Viongozi wengine waliotoa hes-hima za mwisho ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma, Spika wa Bunge Job Ndugai, Naibu Spika Dk. Tulia Ackson na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi.

Wengine ni Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Mabeyo, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Philip Mangula, Katibu Mkuu CCM, Dk. Bashiru Ally, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binillith Mahenge, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Moses Kusiluka, viongozi wa dini, majaji wakiwamo wastaafu, makatibu wakuu na viongozi wa taasisi za serikali na binafsi.

Akimzungumzia marehemu, Mkurugenzi wa Utawala katika Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ben Kabungo, alisema Jaji Nsekela, alikuwa kiongozi mwenye maono na amewafundisha kujenga umoja.

Aidha, alisema alisimamia kanuni za mgongano wa maslahi zikatengenezwa amekuwa akisimamia kanuni kwa uadilifu na kuahidi kuendeleza yote aliyoacha.

"Tumepoteza kiongozi ambaye alikuwa analea na amekuwa kama baba kwetu," alisema.

Naye Katibu Msaidizi, Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Arusha, Anna Mbasha, alisema alikuwa kiongozi, mnyenyekevu na mchapakazi.

"Alipenda haki, kafanya kazi kwa jitihada zote na muda wote ni kiongozi ambaye aliamini hatuwezi kushindwa kusimamia tuliyopanga," alisema.

Awali akisoma wasifu, Katibu Mkuu Ikulu, Moses Kusiluka, alitaja nyadhifa mbalimbali ambazo Jaji Nsekela amezitumikia kuwa ni pamoja na Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ) na Makamu wa Rais wa Mahakama hiyo. Aidha, aliwahi kuwa Rais wa Mahakama ya Afrika Mashariki, pia Mjumbe wa Taasisi ya Waamuzi na hadi mauti inamkuta alikuwa Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.



## Makinda ataka kasi mapambano ya ukatili

**Na Christina Mwakangale**

SPIKA Mstaafu, Anne Makinda, ameitaka jamii kutofumbia macho vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake, wasichana na watoto.

Amesema vitendo hivyo ni kinyume na haki za binadamu, vinaumiza, vinadhalilisha na kuathiri uchumi.

Makinda aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kushirikisha wadau mbalimbali.

"Ushirikiano wa wadau mbalimbali katika kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutokomeza ukatili wa kijinsia ni muhimu, ili kuhakikisha kuwa haki za wanawake na watoto zinazingatiwa.

"Kila mmoja wetu ajitafakari kwa upya katika ngazi ya mtu binafsi, taasisi na serikali juu ya alama gani chanya tunataka kuacha katika jamii zetu ili hata siku moja vizazi vijavyo viweze kusoma taarifa zetu na kuona tulipambana," alisema Makinda.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa ukatili wa kijinsia ni janga linaloigharimu dunia, ikiwamo Tanzania, na kwamba ripoti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2015/16 kupitia Taarifa ya Idadi ya Watu na Afya, inakadiriwa kuwa asilimia 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 wamefanyiwa ukatili.

Makinda alisema takwimu zinaonyesha kundi hilo lilifanyiwa ukatili wa kupigwa, kingono katika kipindi cha maisha yao huku matukio hayo yakiongezeka mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza na Kigoma.

"Kwa ujumla taarifa inaonesha hakuna tofauti kubwa ya mabadiliko katika jamii zetu kuhusu mitazamo na matendo ya jamii zetu kuhusiana na ukatili wa Kijinsia.

Ni dhahiri kuwa bado tuna kazi kubwa ya kuhamasisha jamii zetu kubadili, mila, desturi na fikra na mitazamo inayochochea vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia katika jamii," alisema Makinda.

Pia Makinda alitoa wito kwa wadu kuiunga mkono serikali katika Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 - 2021/22, unaolenga kupunguza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto kwa zaidi ya asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema ukatili wa kijinsia unaathiri taifa kwa ujumla, na kwamba utafiti uliofanywa na Benki ya Duni (WB), unaonyesha kuna upotevu wa uzalishaji unaosababishwa na ukatili wa jinsia kwa asilimia 1.2 ya pato la taifa la Brazili na Tanzania.

Alisema pia inaonyesha kuwa nchi za Afrika zinapoteza zaidi dola za marekani milioni 105 kwa kutokuzingatia usawa wa jinsia.



# Upungufu vitamin A bado ni tatizo

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), imesema moja ya matatizo makubwa ya lishe nchini ni upungufu wa vitamini A.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Chakula na Lishe, Dk. Elifatio Towo, wakati akifungua semina ya waandishi wa habari kuhusu mwezi wa afya na lishe ya mtoto.

Alisema bado elimu inatakiwa kwa jamii ili kuhamasisha wananchi kutumia vyakula vyenye vitamini A kwa watoto, ili kuepukana na matatizo ya lishe duni.

Dk. Towo alisema kwa mujibu wa utafiti wa afya na mgawanyo wa watu wa mwaka 2010 takribani asilimia 33 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano walibainika kuwa na upungufu wa vitamini A mwilini. Alisema upungufu wa vitamini A mwilini husababisha madhara mengi kwa mtoto ikiwemo ukosefu wa kinga mwilini na hivyo mtoto kuwa katika hatari ya kupata magonjwa mara kwa mara, kutoona vizuri katika mwanga hafifu. Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo kuna hatua madhubuti zinapaswa kuchukuliwa ili kudhibiti tatizo la upungufu wa vitamini A.

Aidha, alisema mwezi wa afya na lishe ya mtoto ni mojawapo ya mikakati ya kulinda afya na maendeleo ya mtoto ambapo katika kipindi hiki huduma jumuishi za afya na lishe hutolewa kwà mtoto mwenye umri kuanzia miezi sita hadi miaka mitano.

Alitaja huduma ambazo watazitoa ni kutoa matone ya vitamini A, utoaji wa dawa za kutibu maambukizi ya minyoo, upimaji wa hali ya lishe, utoaji wa ushauri nasaha na kutoa rufaa kwa mtoto anayebainika kuwa na utapiamlo mkali.

"Huduma hizi zimekuwa zilitolewa kila baada ya miezi sita yaani mwezi Juni na Desemba kila mwaka na kuwafikia watoto wengi zaidi. Takribani watoto 8,674,656 walifikiwa na huduma zinatolewa katika mwezi wa Afya ya moto, mwezi Desemba mwaka 2019," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Towo, licha ya jitihada nzuri zinazochukuliwa na serikali katika kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa huduma zinazotolewa katika mwezi wa afya na lishe ya mtoto, bado kuna watoto ambao hawajafikiwa na huduma hizo.

"Kuna haja ya kuendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa huduma hizi ili waweze kuwapeleka watoto wao wenye umri wa miezi sita hadi miaka mitano, kwenye vituo vya kutolea huduma za mwezi wa afya na lishe ya mtoto," alisema Dk.Towo.

Alisema matarajio yao ni kuona Wanahabari watahamasisha na kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa huduma zinazotolewa katika mwezi wa afya na lishe ya mtoto.

# NIT yaishukuru Benki ya Dunia kwa ufadhili mafunzo ya anga

**Na Nwabdishi Wetu**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeishukuru Benki ya Dunia kwa ufadhili wa mafunzo ya anga.

Shukrani hizo zilitolewa jijini Dar es Salaam na Mkuu wa chuo hicho, Mhandisi Prof. Zacharia Mganilwa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

"Tunapoadhimisha Wiki ya Usafiri wa Anga Ulimwenguni, tunaishukuru Benki ya Dunia kwa kukisaidia Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Anga na Operesheni za Usafirishaji Ubora katika Uendeshaji wa mafunzo ya usafiri wa Anga hapa chuoni," alisema.

Prof. Mganilwa pia alisema katika sehemu ya msaada kutoka Mradi wa Mabadiliko na Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika Mashariki (EASTRIP (East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project)), NIT inapaswa kutoa wahitimu 4,500 katika miaka mitano kuanzia 2019 mpaka 2024.

Alisema matarajio ya NIT ni kuvuka lengo lililowekwa la kuhakikisha inatoa wahitimu 4,500 kwa miaka hiyo mitano, lakini kitu kikubwa inachojivunia ni kuwa mpaka hivi sasa wameshaonyesha kuwa watavuka tutavuka lengo kwa kuwa katika mwaka mmoja tu wa miaka miwili ya utekelezaji wa mradi; Chuo hadi sasa kimedahili na kimezalisha wahitimu wanafunzi 2,700.

Alisema mwisho wa mradi huo wa miaka mitano, taasisi 16 kutoka Tanzania na Kenya zinatakiwa angalau ziwe zimezalisha wahitimu 20,000 katika mipango ya mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika taaluma zilizolengwa.

"Tumepokea dola milioni 21.25 za Kimarekani (Sh. bilioni 50) kama msaada wa kifedha kutoka Benki ya Dunia na tutaweza kufanya manunuzi ya ndege tatu za mafunzo, ujenzi wa hosteli za wanafunzi, makazi ya waalimu pamoja na karakana za ndege," alisema Prof. Mganilwa. Kwa mujibu wa Prof. Mganilwa, kupitia mradi wa EASTRIP, NIT itajenga majengo mapya tisa ambayo ni jengo maalum la mafunzo ya wahudumu wa ndani ya ndege, hosteli za wanafunzi wavulana na wasichana, maabara za kisasa za kompyuta, makazi ya wafanyakazi na wanafunzi huko Kilimanjaro pamoja na ujenzi wa karakana za ndege.

"Pia tutajenga karakana za ndege 2 karaka na mbili za ndege, moja katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na nyingine Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA)," alisema.

Alisema pia kwamba nchi kwa sasa ina idadi ndogo sana ya marubani na wahandisi wa ndege; hivyo kupitia mradi wa miaka 5 wa EASTRIP, taifa litakuwa na wataalamu wengi wa kuisadia sekta ya anga.

Mganilwa alisema kuwa Taasisi iko katika hatua za mwisho za mchakato wa kutimiza taratibu zote za kuanza kwa kozi ya mafunzo ya marubani katika mwaka ujao wa masomo.



HABARI KITAIFA

# Mbunge afunguka mazito Uchaguzi Mkuu wa 2020

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE wa Kyela, Ally Jumbe maarufu 'Kinanasi', amesema katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, hakuna mwanamume anayeweza kusimama na kusema alimchangia fedha kufanikisha ushindi wake.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa mji wa Ipinda katika mkutano wake wa kwanza tangu achaguliwe kuwa mbunge wa jimbo hilo.

"Uchaguzi huu nimeendesha mimi kwa hela zangu, hakuna aliyenichangia, wala hakuna mwanamume yeyote atakayesimama akasema alinichangia, ila kila Mwanakyela atasimama kwa sababu alinichangia kwa kunipigia kura, lakini siyo pesa za uchaguzi," alisema.

Aidha, Jumbe alijiapiza kuwa yupo tayari kuweka mikono yake kwenye moto iungue kuliko kuona wakulima wa kokoa wakiendelea kusumbuliwa kwa kukopwa mazao yao bila kulipwa kwa muda mrefu. "Tufanye yale ambayo tunayataka, suala la wakulima kusumbuliwa kuhusu kokoa kusubiri miezi miwili, wiki tatu, wiki nne wakati umeuza sitaki, na katika hili nitaweka mikono yangu niungue, hatuwezi kuteseka ni lazima utafutwe utaratibu mzuri," alisema.

Alisema katika kipindi chake atakachokuwa mbunge atakuwa daraja la kujenga umoja na kuwaomba wananchi kuungana ili kuleta maendeleo ya Ipinda na wilaya nzima ya Kyela.

"Tukitengana ukajisikia wewe ni CUF, NCCR ukaona CCM ni adui yako, Kyela ni moja ardhi hii ni moja hakuna ardhi nyingine tutakayozikwa, wageni wanaokuja tukiwa tofauti watatucheka," alisema. Jumbe alisema yeye kuwa mbunge haina maana kwamba alikuwa mahiri sana na uwezo wa kuwazidi wengine ambao hawakuchaguliwa bali suala hili limetokana na mipango ya Mungu. Imani yangu ni kwamba hakuna mwanaKyela ambaye hakunichagua kwa sababu kura ni siri ya mtu uwe CHADEMA au CUF uwe CCM sasa hivi tunazungumza lugha moja tu tulimchagua Rais Dk. John Magufuli, Kinanasi kuwa mbunge na madiwani sasa uchaguzi umekwisha kila mtu ambaye ni mwana-Kyela ana nafasi sawa kwangu," alisema.

Alisema amejipanga vizuri kuwatumikia wana Kyela wote bila kujali itikadi ya vyama vyao, dini wala kabila.



Wakazi wa Kijiji cha Buira, Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, wakisomba matofali, juzi, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walimu wa Shule ya Msingi Buira, ambapo serikali imetoa Sh. milioni 25 ili kuufanikisha. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Wateja NCBA wakumbukwa msimu sikukuu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NCBA imewazawadia wateja wake Visa Debit na Visa Credit card punguzo la gharama kila wanapofanya manunuzi katika maduka ya GSM Retail msimu huu wa sikukuu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika uzinduzi wa promosheni ya 'Nenda Shopping na punguzo kutoka NCBA' iliyofanyika katika mojawapo ya maduka hayo, Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi na wa Kati wa benki hiyo, Julius Konyani, alisema promosheni hiyo ni sehemu ya utamaduni wao wa kuwaheshimu na kuwazawadia ili kuhamasisha wateja wafikie malengo yao.

"Wateja wetu watapata punguzo la bei la asilimia 10 papo kwa hapo, kila mara watakapofanya manunuzi ya Sh. 150,000 au zaidi na kutumia kadi zao za NCBA VISA Debit na NCBA Credit card kwa kufanya malipo katika maduka ya GSM Retail," alisema.

Naye, Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Utaifa wa Benki ya NCBA, Caroline Mbaga, aliongeza kuwa lengo la promosheni hiyo ni kuongeza matumizi ya malipo kwa njia za kidigitali kama njia ya uhakika, salama na rahisi kufanya malipo kote duniani.

"Katika msimu huu wa sikukuu, msimu wa furaha, utulivu, kugawa zawadi na kujenga kumbukumbu za kudumu na unaowapenda; NCBA tunarudisha shukrani zetu kwa wateja wetu ambao wanatumia mifumo ya kidigitali kufanya malipo,"alisema.

Ofisa Masoko wa GSM Retail, Fatma Farah, alisema promosheni hiyo inahusu maduka ya GSM Retail yaliyopo Msasani, Mlimani City, Aura Mall na barabara ya Pugu jijini Dar es Salaam pamoja na miji ya Dodoma na Arusha.

# TBS yatumia maonyesho kuelimisha wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetumia maonyesho ya tano ya bidhaa za viwanda vya Tanzania kutoa elimu kwa wadau.

Miongoni mwa wadau hao ni wazalishaji, wajasiriamali na wananchi kuhusu umuhimu na viwango, faida ya kutumia bidhaa zenye ubora pamoja na kutatua changamoto zao.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho hayo yanayofanyika kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam jana maarufu kama Sabasaba, Ofisa Uhusiano wa TBS, Neema Mtemvu, alisema maonyesho hayo pia yamekuwa fursa muhimu ya wao kusikiliza maoni ya wadau hao.

"Lakini pia tumetumia maonyesho hayo kuwaeleza washiriki, wazalishaji na wananchi kuhusiana na faida ya kupata alama ya ubora," alisema Mtemvu.

Mtemvu alisema wazalishaji wakipata alama ya ubora, wanaweza kufikia masoko mbalimbali hasa ya Afrika Mashariki na zitaweza kuvuka mipaka ya nchi hizo bila vikwazo vyovyote.

"Hii ni kwa sababu katika nchi za Afrika Mashariki tumeoanisha viwango vyetu, mfano bidhaa ikitoka Tanzania kwenda Rwanda kama ina alama ya ubora inapaswa kupita bila kupimwa," alisema.

Kwa upande wa wajasiriamali, alisema wanatumia maonyesho hayo kuwaeleza kuwa huduma ya kupata alama ya ubora bure bado ipo, hivyo wanakaribishwa kuchangamkia fursa hiyo.

"Tunawakaribisha TBS wanachotakiwa kufanya ni wao kupitia SIDO kwa ajili ya kupata barua ya utambulisho, hivyo wakishawaleta kwetu tunawapatia huduma ya kupata alama hiyo ya ubora," alifafanua.

Kwa upande wa wananchi, Mtemvu alisema wanawasisitiza pale wanapoenda kununua bidhaa waangalie kama zina alama ya ubora, tarehe ya mwisho wa muda wa matumizi kwa ajili ya kulinda afya zao na thamani ya fedha zao.

Kuhusu wafanyabiashara, alisema TBS inawahimiza wahakikishe wanazalisha bidhaa zilizo na ubora hatua itakayosaidia kulinda mitaji yao na kuhimili ushindani kwenye soko.

# Sababu fedha za ruzuku kwa vijana kurejeshwa halmashauri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWITIKIO mdogo wa vijana wakulima wenye uwezo wa kulima kuanzia hekari tano na kuendelea katika Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, umesababisha Halmashauri kuendelea kubaki na fedha za kununua ruzuku za pembejeo ambazo zimekuwa zikitengwa kila mwaka.

Halmashauri hiyo katika msimu huu wa kilimo imetenga Sh. Milioni 72 za kununa ruzuku za pembejeo na kuzigara bure kwa wakulima vijana, lakini zimetumia kiasi cha Sh. milioni 24 pekee na kusababisha Halmashauri kuendelea kubaki na fedha hizo.

Akikabidhi ruzuku hizo juzi, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, alisema lengo la utaoji wa ruzuku kwa vijana hao ni kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana na kuondokana na changamoto ya ukosefu wa pembejeo za kilimo.

Alisema moja ya sababu ya vijana kushindwa kujitokeza kwa wingi kuchangamkia frusa ya pembejeo bure ni kutaka kupewa fedha hizo wakanunua wao pembejeo, hali ambayo watazielekeza kwenye kubeti badala ya kuzielekeza shambani kama zinavyotakiwa kutumika.

Alisema kila mwaka wa fedha amekuwa akitenga fedha kwa ajili ya kununua ruzuku za kilimo kwa vijana na mwaka huu ametenga Sh. milioni 72, na kwamba kati ya fedha hizo, Sh. milioni 24 ndizo zimetumika kununua pembejo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana 545.

Aidha alisema mwaka jana Halmashauri ilitenga Sh. milioni 54 na kutumika Sh. milioni 14.19 pekee, hivyo kuwataka vijana wenye uwezo wa kulima hekari tano kujitokeza katika ofisi za serikali za vijiji na kata kwa ajili ya kupata pembejo.

Nae Ofisa Kilimo wa Halmashauri hiyo, Samson Sumuni, alisema wakulima 545 wa mazao ya chakula na biashara wamepatiwa ruzuku za pembejeo za kilimo bure, na wanataraji kulima zaidi ya hekari 725, huku hekari 500 zikiwa za zao la mtama.

Sumuni alizitaja pembejeo hizo ni mahindi kilo 785, aliezeti 45, dawa za pamba chupa 20, mbolea za kupandia na kukuzia mifuko 225 na mbengu za mtama kilo 1,500 ambazo zitagawiwa kwa wakulima waliko kwenye kata 15 zinazoshiriki kilimo pekee.

Elizabeth James, mkulima kutoka Kata ya Kinaga, alisema kabla ya kuwapatia pembejeo hizo walikuwa wakitumia samadi wakati wa kilimo na kusababisha kupata mavuno kidogo.



Mtaalamu wa Mawasiliano na Ubia wa Ezypesa, Eunice Herbet, akizungumza na mawakala wa huduma ya Ezypesa, kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo kuzingatia taratibu ili huduma hiyo iwe na tija, wakati wa warsha iliyowakutanisha mawakala wote wa Zantel, Mkoa wa Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yataka uwekezaji zaidi mafunzo ya bima

**Na Mwandishi Wetu**

CHANGAMOTO za upatikanaji wa huduma mwafaka za bima nchini zitapata ufumbuzi kutokana na uwapo na wataamu wenye mafunzo stahiki kwa ajili ya kuzifanyia kazi na kusaidia maendeleo ya sekta hiyo.

Hiyo ilibainishwa na Kamishna wa Bima, Dk. Mussa Juma, ambaye aliwataka watoa huduma hizo wote kuwekeza zaidi katika mafunzo na elimu ya bima kwa wafanyakazi wao ili waweze kulihudumia soko kikamilifu na kusaidia kubuni bidhaa zinazoendana na mahitaji ya taifa na mazingira ya nchi yetu.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya maafisa bima wa Benki ya NMB, Dk. Juma alisema uwekezaji huo utayasaidia kampuni za bima, benki zinazofanya biashara hiyo, mawakala na wadau wengine kuwa na wafanyakazi wenye sifa za kitaaluma katika tasnia hiyo.

Alisema kada hiyo ya wataalamu ni muhimu si tu katika kurahisisha ukataji wa bima na upatikanaji wake bali pia kwenye kusaidia kuwapo kwa bidhaa sahihi sokoni pamoja na kuongeza uwezo wa kuwahudumia wananchi.

Pia alisema watashiriki kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo ikiwemo mchango mdogo kwenye uchumi na maendeleo ya nchi, alifafanua kiongozi huyo wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

"Sheria ya Bima inataka kila mtoa bima, awe benki au hata wakala yeyote wa bima, anatakiwa kufanya mafunzo kwa watoa huduma wake. Nawapongeza NMB kwa kuzingatia hilo na sisi kama wasimamizi tutahakikisha mnapata msaada mnaotaka ili kusogeza huduma za bima kwa Watanzania wengi zaidi," Dk. Juma alisisitiza katika hotuba yake ya ufunguzi wa mafunzo hayo.

"Kuingia kwa Benki ya NMB kwenye bancassurance ni ushindi mkubwa kwa sisi tulioko kwenye sekta ya bima nchini, kwani kwa miezi michache tu tumeshaanza kuona mabadiliko ya utoaji huduma pia watu wengi wamepata ahueni kwani Benki ya NMB imesambaa kila kona ya nchi hii, bara na hapa Zanzibar," aliongeza.

Taasisi hiyo ya fedha nchini ilianza kutoa huduma za bima mwezi Februari mwaka huu ikiwa ni benki ya kwanza kuanza rasmi kufanya biashara hiyo ijulikanayo kitaaluma kama bancassurance.

## Madiwani wapewa kazi ya udhibiti fedha za umma

**Na Vincent Tiganya,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amewataka madiwani kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma ili ziweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa ya kuwasaidia ya kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Alisema fedha zote ni lazima zitumike kwa kuzingatia mipango na bajeti za Halmashauri na Serikali kwa ujumla kupitia sheria ya bajeti na ya fedha za umma.

Dk. Sengati alitoa kauli hiyo jana wakati wa uzinduzi wa Baraza jipya ya Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Alisema madiwani wanalo jukumu la kuhakikisha fedha zote zinazopelekwa na Serikali Kuu na walizokusanya zinatumika kwa usahihi na uwazi na kuzipeleka katika shughuli mbalimbali za wananchi.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema hatua hiyo itasaidia kuepuka matumizi yasiliyokuwamo katika bajeti waliyopitisha ambayo yanarudisha nyuma maendeleo na kuwasononesha wananchi.

Alisema ili kudhibiti ufujaji wa makusanyo ya Halmashauri, ni lazima fedha zote zikusanywe kwa kutumia mashine na kutoa stakabadhi kwa waliotoa fedha.

Alisema ni marufuku kwa watendaji waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kutumia vitabu kuandika kwa mkono wakati wa makusanyo ya mapato ya Halmashauri kwa kuwa njia hiyo ndio inayotumika kuiba fedha za umma kwa kutoa taarifa zisizosahihi za ukusanyaji wa fedha.

Mkuu huyo wa Mkoa aliongeza kuwa Madiwani wanalo jukumu la kuhakikisha kuwa hakuna fedha inayotumika kabla ya kupelekwa benki.

Alisema utumiaji wa fedha ambazo hazipiti Benki (fedha mbichi) unasababisha kuzalishwa kwa hoja za kiugazi na wakati watendaji wasio waadilifu kutumia nafasi hiyo kuiba fedha za umma.

Aidha Mkuu huyo wa Mkoa aliwataka Madiwani kuhakikisha wanasimamia na kuwahimiza watendaji katika maeneo yao kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuiwezesha Manispaa ya Tabora kuwa na fedha nyingi zitakazosaidia katika shughuli za maendeleo ya wananchi.

Alisema ni lazima wajipange kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2025 wanakuwa na mapato ambayo watakuwa tena hawategemei fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Katika hatua nyingine Madiwani wa Manispaa ya Tabora wamemchagua Diwani wa Kata ya Isevya, Ramadhan Kapera kuwa Meya .

Taifa laendelea 'kukalia' uchumi wa bahari kuu

Ukurasa 13




siasa

JUMATANO DESEMBA 9, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 14

**Kilichomvusha Mwalimu Nyerere kung'arisha nchi ndani ya miaka 10 uhuru wa Tanzania**

MIAKA 59 YA UHURU

# Namna Mwalimu Nyerere, Kawawa walikutana wakadumu 'damu damu'

• Kabla na baada uhuru, hadi wastaafu

**Na Peter Orwa**

KATIKA siku zilizopita walioshuhudia zama za uongozi wao, wajihi wa uhusiano wa Mwalimu Julius Nyerere na Rashid Kawawa, ulibeba sura ya kindugu, hata katika mwonekano mbele ya umma.

Iko wazi, Rais Nyerere alimtumia sana Waziri Mkuu Kawawa hasa katika katika zama za uongozi wake wa uwaziri mkuu na baadaye sana, Katibu Mkuu wa chama - CCM kufanikisha ajenda za kitaifa.

Kawawa alidumu kuwa 'jembe na mwadilifu wa Nyerere' aliyejulikana kitaifa katika utekelezaji kuanzia itikadi hadi 'hapa kazi,'hata kuna wakati alipokuwa katika nafasi nyinginezo za uwaziri, akiwamo asiye na wizara maalum.

Ulikuwa ufanyaji kazi wa timu halisi na hata watoto ngazi ya shule wakati huo siasa ya chama kimoja, kuna ushuhuda wa mengi hata katika mazuri ya kujifananisha katika staili yao michezoni "Mimi Nyerere na wewe Kawawa."

Ikumbukwe ni zama ambazo mfumo wa chama kimoja ulikuwa juu na itikadi ya nchi, Ujamaa na Kujitegemea, ulijenga kasi, wakubwa kwa watoto waliofautilia kuanzia shule hadi redioni walifahamu vyema na baadhi wakiwa katika matamshi duni ya kujifunza '...kujimetegea.'

Mwanzo wa watu hao kukutana na hata 'wakaiva' kiutendaji mzizi wake uko wapi? Ni aina ya majibu yaliyochukua muda kutafutwa, hadi katika zama ambazo wote hawakuwa madarakani na mengine zaidi ya hayo.

Wakati mfumo wa vyama vingi vinaanza tena mwaka 1992 baada ya kutoweka mwaka 1964, Mwalimu Nyerere alishawahi kutoa kauli nzito



Rais Julius Nyerere na Rashid Kawawa, katika zama za mwanzo wa uhuru wa nchi. **PICHA: MTANDAO.**

pale aliposhindwa kukubali alichokitafsiri ni namna ya kejeli kutoka kwa aliyekuwa kiongozi wa nchi katika miaka 10 ya mwanzo wa uhuru.

Nyerere alitamka "angeniambia mimi tu nisingemjali sana, lakini kamkashifu Rashidi (Kawawa)... sitakubali, nitamshitaki!"Ilikuwa kauli nzito na iliyoonyesha thamani ya Kawawa na hata sura ya upendo wenye undugu wa kihistoria.

Msingi wa tamko hilo unaweza kuuganishwa na ushuhuda wa mwaka 2006 wilayani Tunduru, wakazi wake walipompokea Mzee Kawawa katika Uwanja Mdogo wa Ndege wa Misheni ya Mbesa, kwa ajili ya kuzindua kampeni za uchaguzi mdogo.

Kawawa alipokaribishwa katika chumba cha wageni, walimuimbia wimbo mkongwe "...eeh eeh TANU yajenga nchi..." ambao ulitawala sana katika zama za mwanzo za uongozi wa Mwalimu Nyerere, Ujamaa 'ukiwa mbichi.'

Badala ya kuungana nao walau kwa kutikisa kichwa au tabasamu, Kawawa alishindwa kujizuia kwa kutokwa machozi, hali iliyowafanya waimbaji kukatisha na wengi katika hadhira, fikra zilienda mbali kwa mtazamo "amekumbushwa mbali kwa kina Nyerere."

Aliyekuwa Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam marehemu, Kapteni mstaafu John Barongo, aliwahi kutoa angalizo la ki-uanahabari, alipotaka historia ya wakongwe wa nchi zikawekwa sawa kabla hawajaondoka, kazi aliyofanya kwa mdomo na alirudia kwa andiko gazetini.

Naam! Niliamua kulichukulia kwa uzito stahiki, kuunganisha na kama hicho kilichowahi kunivutia miaka mingi redioni kutoka kwa aliyekuwa mwanataaluma wa historia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu Huria (OUT), Profesa Joseph Mbwiliza.

Mtaaluma huyo aliyewahi kukalia wadhifa naibu waziri kwa tiketi ya ubunge Kasulu na wakati fulani Mkuu wa Chuo cha CCM Kivukoni, alihimiza maboresho ya historia taifa, ulivyokuwa mkakati wa UDSM kutaka kutafiti wa kuweka sawa historia ya jamii ya Hadimu, visiwani Zanzibar.

Kimsingi, inaangukia kundi lile lile la wazo la Kapteni mstaafu Barongo. Hapo ndipo nami nikajiwekea ajenda ya kujua historia kufahamu siri ya muugano wenye ufanisi kiongozi, kati ya Mwalimu Nyerere na Mzee Kawawa.

**MZIZI WA UHUSIANO**

Wazungu wana usemi 'getting from the horse's mouth' kwa maana ya uhalisia unatoka kwa mhusika. Ni utekelezaji uliofanyikia muda mfupi baada ya kifo cha Mwalimu Nyerere, wakati kila pande wakidodosa kihistoria.

Mwanzo wa kazi hiyo ilikuwa faragha ya saa tatu na Mzee Kawawa nyumbani kwake Madale, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam na nyingine kama hiyo kwenye tukio la kumbukumbu la mwaka tofauti, nili-

INAENDELEA UK. 12

# Namna Mwalimu Nyerere, Kawawa walikutana wakadumu 'damu damu'

INATOKA UK. 11

fungia safari kumfuata Mama Maria Nyerere, kwake kijijini Butiama, Mara.

Swali mojawapo lililomuangukia Mzee Kawawa ni kupata mzizi na siri ya ukaribu wao na Mwalimu Nyerere, uliodumu milele.

Ni swali ambalo dhahiri lilichangamsha mazungumzo yetu, kwa namna ya pekee. Kwanza alitabasamu, kubadili staili za mkao, aliivua kofia na kuiweka sawa, ikiwa ishara za wazi kujiandaa kujibu swali alilolipenda.

Akiwa katika hali ya ugonjwa wakati huo takriban miaka 20 imepita, Mzee Kawawa alisimulia mwanzo wake kwamba alipokuwa anasoma shule ya sekondari mkoani Tabora, kuna siku walikusanyika na wanafunzi wa shule nyingine kujadili mada ya kitaaluma maarufu 'debate.'

Alisema, wanafunzi wenzao walifika na walimu wao, akiwamo Nyerere na (Balozi) Tibandebage, ambao hafichi umahiri wao katika kuwafanyia maboresho kitaaluma au 'moderation' ilimkosha sana.

Mzee Kawawa alimnyooshea Mwalimu Nyerere kidole cha pekee, namna alivyojenga hoja, sanaa ya lugha na sauti binafsi vilivyomgusa sana, hata tangu wakati huo akawa anavutiwa naye sana, pasipo Mwalimu Nyerere kujijua.

Alisema, baada ya kumaliza masomo aliajiriwa na kushiriki katika harakati za wafanyakazi na hadi mwaka 1955, alishakuwa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanganyika (TFL).

Upekee wa Kawawa unakumbukwa sana alipoandaa migomo iliyotikisa sana serikali ya kikoloni na katika nafasi ya kipekee kampuni ya bia, Dar es Salaam na ile ya Shirika al Reli mjini Tabora, chini ya kiongozi wao, Christopher Kasanga - Tumbo.

Wakati huo, Nyerere alishaacha ualimu akiwa rasmi ana mwaka mmoja katika uongozi wa chama cha TANU kuendesha harakati za kusaka uhuru, naye alivutiwa sana na kijana aliyemsikia wakati huo, Rashidi Kawawa, namna alivyowatikisa watawala kudai haki ya watumishi.

Hapo ndipo Nyerere aliamua kumtafuta mwaka huo wa 1955 na wakakutana katika jengo la makao makuu ya TANU, jijini Dar es Salaam (sasa ofisi ndogo ya CCM, Lumumba), rai kuu ya Mwalimu ni washirikiane na Kawawa kuibana serikali ya kikoloni kupata uhuru.

"Wakati anajitambulisha na kuniomba tushirikiane, angejua mimi nilikuwa namfahamu, nampenda na nimeshakubali siku nyingi!" alisimulia Kawawa na kucheka kuhusu kumbukumbu hiyo, kwa wakati huo ilishadumu zaidi ya miaka 45.

Alisema tangu wakati huo Chama cha Wafanyakazi na TANU vikaingia ubia wa siri katika harakati za siri kuwabana wakoloni na baada ya miaka kadhaa, Nyerere alimshawishi ahamie rasmi TANU.

Ndio ukawa mwanzo wa mageuzi, Kawawa kupewa cheo akiwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO) kwa tiketi ya TANU, ambako nako alipata nafasi muhimu.



Waasisi wa TANU, kutoka kushoto ni Sheikh Suleiman Takadir, Mbutta Milando, John Rupia na Julius Nyerere. Waliowazunguka na silaha za jadi ni Bantu Group, kundi la vijana wa chama ulinzi kwa viongozi hao, mwaka 1955.

Pia, ni safari ambayo muda mfupi baada ya uhuru, Kawawa aliaminika sana kwa Nyerere, pale alipoachiwa uongozi wa nchi kwa muda na Mwalimu Nyerere, akirejea TANU kwenda kuimarisha chama.

Mfumo wa kuleta vikundi au wanajamii jirani, ilikuwa mbinu mojawapo ya kuimarisha TANU, kwani ni wakati huo Nyerere alishirikiana na kinamama wajasiriamali wa Kariakoo, hata akampata 'jembe' Bibi Titi na Lushoto alishirikiana na wanajamii, kusumu safari ya Uhuru.

**MAMA MARIA?**

Akizungumza katika faragha kwa lengo lilelile kama Kawawa, mjane Mama Maria Nyerere, aliendeleza ufafanuzi kuhusu mbinu hiyo ya kusaka uhuru, namna vikundi vya vijana vilishiriki katika harakati za siri kushinikiza uhuru.

Mama Maria, alitaja katika nafasi ya pekee jijini Dar es Salaam vikundi vya vijana na klabu kubwa ya soka ya Yanga iliyoko Jangwani, ilitumika kuratibu vijana, akimtaja kwa upekee mdogo wa Mwalimu Nyerere, marehemu Joseph Nyerere, mdau mwandamizi.

Kuhusu uhusiano kuchukua sura ya undugu na Kawawa, Mama Maria, alisema walishaishi jirani katika hali iliyokomaza uhusiano hadi katika sura ya mwafamilia mmoja mmoja, kati ya pande hizo mbili.

Alisema, ni namna ambayo iliendа mbali hata katika uhusiano ndani ya chama TANU, kwamba walitafuatiana washenga wa vijana wao kuoa ndani ya wajumbe wa vyombo vya chama kama vile halmashauri za TANU.

"Tunasema huyu kijana wetu anaenda kwa wachagga, nani anaweza... aah! (Sir George) Kahama unawaweza, tukutume!" alitamka katika lugha ya mfano.

Ni aina ya uhusiano ambayo ilizaa ushuhuda uliotetewa na wote wawili, Kawawa na Mama Maria, uhusiano baina yao, watoto wa kila upande kuita mwingine kwa heshima rasmi ya wazazi wao.

Mama Maria aliendelea kwamba, hata viongozi wakuu wengine wa nchi, walifungwa na ukaribu uliiopitiza hadi ngazi ya familia.

Katika ufafanuzi wake, namna kulivyokuwapo mwitiko mkubwa wa wa familia ya Kawawa katika msiba wa Baba wa Taifa, Mama Maria alidokeza: "Yule (Nyerere) ni baba yao (watoto wa Kawawa )."

**MISUGUANO KICHAMA?**

Wakati wa mazungumzo na Mzee Kawawa, kuna hoja iliyoibuliwa na mwandishi kutaka kujua kulikoni migogoro ya siasa iliyoonekana wakati huo wa mazungumzo (hali inayojiri hata sasa), kutoka baadhi ya vyama vya siasa, akitaka ulinganishaji na TANU, hata CCM ya zama zao.

Kawawa alifafanua kwamba, msuguano ndani ya vikao vyao si jambo geni, ila tofauti aliyoieleza ni katika namna makubaliano yanavyofikiwa na kusimamiwa kama jambo la ndani kichama.

Alisema vikao vya TANU na baadaye CCM vilijenga tabia, hata ilipotokea misuguano mikali, daima walimaliza kwa ajenda walizokubaliana na wote walisimama katika mstari wa kuzitetea baada ya kikao, jambo aliloeleza kusikitishwa anaposhuhudia inatoweka kwa vyama vingi vilivyoibuliwa baadaye.

Siku la leo wakati Watanzania wanaadhimisha Miaka 59 ya Uhuru wao, kuna mengi ya kuenziwa kutoka kwa waasisi hao wa Taifa waliokwishatangulia mbele ya haki.

• ***Ijumaa ijayo usikose makala namna mpango wa kwanza wa uchumi baada ya uhuru unavyoshikilia kanuni zinazoendesha uchumi hadi leo nchini. Pia, Jumamosi, usikose simulizi za swahiba mkuu wa Mwalimu Julius Nyerere, kila alipokuwa nje ya ofisi, tangu zama za umri mdogo kabla uhuru.***




Mwalimu Nyerere, akifurahia jambo siku ya uhuru wa Tanganyika. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MIAKA 59 YA UHURU**

# Taifa laendelea 'kukalia' uchumi wa bahari kuu

## •Lakosa viwanda kuchakata minofu
## •Maelfu tani za samaki yauzwa ghafi



Samaki wakubwa duniani 'marlin' na 'barracuda' ni miongoni mwa viumbe bahari wa kipekee vinaopatikana kwenye bahari kuu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NI miaka 59 ya uhuru uliopatikana Desemba 9, mwaka 1961 kutoka kwa Mwingereza. Ni zaidi ya nusu karne sasa tangu ukombozi huo, lakini si Tanzania Bara wala Visiwani iliyotumia fursa za uchumi wa 'buluu' au rasilimali bahari inayoizunguka.

Hali ni tofauti kwa nchi zilizoendelea kama Marekani na mataifa mengine kama China ambayo yamewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye uchumi wa buluu.

Makadirio ya ukubwa wa jumla wa meli za uvuvi za China zilizopo katika maji ya mataifa mbalimbali duniani ni nyingi. Inaelezwa kuwa ina boti za uvuvi kati ya 200,000 hadi 800,000, zikishughulikia karibu nusu ya shughuli za uvuvi duniani.

**UCHUMI WA BULUU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu, Dk. Islam Seif, anazungumza na Nipashe na kueleza kuwa unahusisha shughuli zote za kiuchumi zinazofanyika baharini na pwani.

"Ni pamoja na uvuvi, ufugaji samaki, uchimbaji mafuta na gesi, uhandisi wa bahari, usafirishaji, utalii, bandari na madini. Yote ni matumizi ya rasilimali bahari yanayokwenda pamoja na uhifadhi wa urithi huo," anasema Dk. Islam.

**KUCHELEWA KUNUFAIKA**

Dk. Islam anasema taifa halijanufaika kikamilifu kutokana na kukosa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya baharini hasa samaki. Hali hiyo inadhoofisha maendeleo ya sekta ya buluu kwani hakuna uchakataji wa minofu ya samaki.

"Mathalani, wastani wa samaki wanaovuliwa kwa mwaka ni tani 8,000 hadi 17,000, lakini wote huuzwa wakiwa ghafi."

Anasema uwekezaji kwenye bahari kuu ulianza baada ya mataifa yaliyoendelea kuwekeza kwa wingi katika sekta ya anga na nchi kavu, yaliona kuna fursa ya uwekezaji katika bahari ambayo haijatumiwa kikamilifu hivyo Zanzibar na Tanzania zikaona wakati umefika kuwekeza katika uchumi huu badala ya kuweka mkazo zaidi sekta ya utalii.

Anasema Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Hussein Ali Mwinyi, moja ya kipaumbele chake ni uchumi wa buluu hasa uvuvi.

"Nadhani muda wa kuitumia bahari kikamilifu ulikuwa haujafika kwa sababu ukiangalia mipango yote ya maendeleo ya nchi zetu, kuna mipango ya kujenga bandari, viwanda vya mwani na kuimarisha usafiri wa baharini," anasema Dk. Islam.

**MAFANIKIO**

Benki ya Dunia inautaja uchumi wa buluu kama matumizi endelevu ya rasilimali za bahari kwa ukuaji wa uchumi.

> Mapato yanagawanywa kwa Zanzibar asilimia 20 na Bara 30 na nusu iliyobakia kwenye shughuli za mamlaka," anaongeza Dk. Islam.

Kwa tafsiri hiyo, Dk. Islam anasema uvuvi unachukua nafasi kubwa na ili kuimarisha sekta hiyo Serikali ya Muungano, ilianzisha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari.

"Mafanikio yanaanza kuonekana ikiwamo kuanzishwa wa sheria ya mwaka 2020 inayoondoa mivutano baina ya pande mbili za Muungano,"anasema.

Aidha, anasema mamlaka imepunguza uvunaji haramu wa rasilimali za baharini unaofanywa na meli za kigeni.

"Kuna kesi zaidi ya 12 za meli zilizokamatwa zikivua katika bahari yetu lakini kuanzia 2016 hadi 2017 kuna meli sita zilizokamatwa na kutozwa faini ya zaidi ya dola 200,000," anasema.

Mbali ya kudhibiti uvuvi haramu kwa teknolojia ya kisasa, mamlaka imeuza leseni za uvuvi wa bahari kuu 474 kuanzia mwaka 2010 na kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 3.0 kwa mwaka.

"Mapato yanagawanywa kwa Zanzibar asilimia 20 na Bara 30 na nusu iliyobakia kwenye shughuli za mamlaka," anaongeza Dk. Islam.

Anasema zamani mamlaka ilitegemea mauzo ya leseni kwa meli za kigeni, lakini karibuni kuna meli nyingi zinazomilikiwa na wazawa zinazoomba leseni ya kuvua bahari kuu.

"Serikali inatarajia kununua meli nyingine nane za uvuvi ambazo naamini zitaongeza mapato na kuzalisha ajira kwa vijana," anasema.

Anasema meli za wazawa zinavua jodari, sehewa na nduwaro na soko kubwa lipo Bara na kwamba kampuni ya Salmin ya Uturuki imetangaza uwekezaji mkubwa wa zaidi ya Sh. trilioni 6.0 kwenye uvuvi wa bahari kuu.

**MAONI YA WIZARA**

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi wa Zanzibar, Abdullah Hussein Kombo, anasema Zanzibar itabadili uchumi wake kupitia sekta hiyo na kuwekeza zaidi katika uvuvi wa bahari kuu badala ya utalii pekee.

Mkurugenzi wa Shirika la Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) Zahor Kassim, anaongeza kuwa shirika hilo lina miradi ya kuendeleza uvuvi ikiwamo kujenga kiwanda cha kuchakata samaki chenye uwezo wa kusindika tani 20 za samaki kwa siku na pia kitakuwa na eneo la kuhifadhi tani nyingine 1,500.

**CHANGAMOTO**

Licha ya mafanikio yaliyoanza kuonekana katika sekta ya uvuvi kuna maeneo magumu ya kupitia kabla ya kufikia mafanikio ya kweli, anasema Dk. Islam.

Uharibifu wa mazingira unaofanywa na meli za kigeni kinyume na masharti wanayopewa wanapoomba leseni ni changamoto nyingine.


"Nyingine huvua samaki wadogo na kuwatupa kwa kuogopa kuchukuliwa hatua ingawa changamoto hii tumeanza kuidhibiti kwa kuwafuatilia."

Anachoshauri Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu, Dk. Islam Seif, ni wawekezaji katika sekta hiyo kuwa wabunifu na kuacha kuvua kwa mazoea.

"Uvuvi wa bahari kuu una gharama kubwa, sasa kama utavua kwa mazoea huwezi kuona faida yake lakini pia serikali ziwekeze katika ujenzi wa miundombinu ikiwamo meli za kisasa za uvuvi na bandari za samaki."

> Nyingine huvua samaki wadogo na kuwatupa kwa kuogopa kuchukuliwa hatua ingawa changamoto hii tumeanza kuidhibiti kwa kuwafuatilia."

# Kilichomvusha Mwalimu Nyerere kung'arisha nchi ndani ya miaka 10 uhuru wa Tanzania



Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

**Na Sabato Kasika**

NI siku ya tabasamu la ushuhuda wa miaka 59 ya uhuru wa nchi, iliyoanza na jina Tanganyika wakati huo. Miaka miwili na miezi kadhaa baadaye, ukaundwa udugu wa kudumu na majirani Zanzibar, hata kicheko kikazidi kufurahia muungano uitwao Tanzania.

Daima, kumbukumbu ya siku ile ya kwanza na kuendelea, ilipozaliwa Tanganyika huru, ni vigumu kutenganisha historia inayowahusu raia wengi, lakini kwa upekee shujaa anayedumu kuwa nembo wao, Mwalimu Julius Kamabarage Nyerere, ambaye wasifu wake una kishangilio, Baba wa Taifa.

Inakuwaje mpaka anabeba sifa hiyo? Waswahili wanasema, 'usione vyaelea, vimeundwa', Kimsingi ana mengi; Alikuwa mzalendo, muadilifu, mwenye nidhamu, mchapakazi, mbunifu, moyo wa kujitolea na mshirikishaji wa mambo ya kitaifa, kuanzia kiserikali hadi chama.

Ni sehemu ya wasifu unaomfanya kuwa usukani wa yanayoing'arisha Tanzania ya leo katika picha pana ya kimaendeleo, kwa mantiki mtambuka, akishirikiana na timu kuu ya wenzake kwa karibu, pasipo kusahau marafiki alioungana nao kimataifa. Hulka yake mojawapo kwa maneno na vitendo, aliwahimiza watu wafanye kazi bila ya kusukumwa ili kujiletea maendeleo katika taifa lao huru, binafsi na katika vikundi, ambako aliamini ni rahisi kuwekeza mahitaji yao ya maendeleo.

Katika ujenzi wa Tanganyika na baadaye Tanzania, hususan mwaka 1964, alijiamini na anachokifanya na hata akajigamba wazi kwa kuwakaribisha wakoloni baada ya miaka 10 ya uhuru, yaani 1971, wafike kushuhudia hatua kubwa iliyofikiwa kwa maendeleo ya Watanzania.

Kwa vijana wa enzi hizo, ambao ni wazee wa sasa, wana kumbukumbu vyema ya bendi ya Moro Jazz na kinara wao Mbaraka Mwishehe Mwaruka, walipohimiza tamko la Mwalimu kwa kutunga kibao cha 'Miaka 10 ya Uhuru' ambacho kilikuwa na orodha ya mafanikio lukuki kitaifa.

**NINI KILICHOVUNWA?**

Sura kuu ya kwanza kimaendeleo, iko katika tathmini ya uhai wa mwanadamu na manufaa yanayoendana nayo. Naam! Mara moja vifo vya watoto wanaozaliwa vilipungua maradufu ndani ya miongo miwili, kuanzia mkakati ulipoanza mwaka 1965, ikiwa ndio kipindi cha kwanza cha mpango wa maendeleo ya nchi, ilikuwa na muda mfupi.

Halikadhalika, kuna ushuhuda chanya wa mikakati kwa umri wa kuishi uliongezeka, kutoka wastani wa miaka 37 katika kipindi cha mwaka mmoja kabla ya uhuru, hadi 52 ilipotimu miaka 1984. Uandikishaji wa wanafunzi katika shule ya msingi nao ulisogea kutoka asilimia 25 kwa watoto wa kike, katika zama hizo zilizotajwa hadi kufikia asilimia 72 kwa mwaka 1985.

Watu wazima ambao hawakujua kusoma na kuandika, kupitia mikakati ya elimu kwa watu wazima, ambayo kimsingi iliundiwa taasisi maalum, nao idadi yao kutoka asilimia 17 wakati wanasherehekea uhuru, hadi asilimia 63 wakati walijinasibu miaka 14 ya uhuru wao.

Kimataifa, Tanzania huru ilishajichimbia mizizi mirefu ya urafiki, ukiondoa ndugu zake wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) mzaliwa wa mwaka 1963,

> Maudhui ya tamko hilo yalibeba sura kuu tano ambazo ni makusudio yanayosomeka: "Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, tumepuuzwa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka mapinduzi, mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena, tusinyonywe tena na tusipuuzwe tena".

ng'ambo ya Mashiriki walikuwapo wanandugu kama iliyokuwa Umoja wa Nchi za Kisovieti (USSR), Cuba na namna ya kipekee, Jamhuri ya Watu wa China.

Ni hatua urafiki wa kihistoria uliwaunganishwa Watanzania na Wachina, Mwalimu Nyerere akiwa swahiba mkubwa wa kiongozi wao, Mao Tsetung, mgongoni kwao, utekelezaji wa yote ya msingi yaliyodumisha urafiki huo kwa niaba ya nchi hizo mbili, ulishuhudiwa uchapakazi wa kipekee wa watendaji wao waandamizi kitaifa, mawaziri wakuu, Rashid Kawawa na Chuo En Lai.

Inakumbusha historia ya wasaidizi hao kuiva kikazi na binafsi, hata Kawawa, alizama kuhusudi mavazi ya Kichina, shati lisilo na kola, huku katikati ya miaka ya 1960 Watanzania wakishuhudia mazao ya ujenzi wa zahanati zinazofanana kama za Temeke, Mwananyamala, Amana, Mnazi Mmoja na Magomeni, mjini Dar es Salaam, Mwere Morogoro na Chumbageni Tanga.

Kupitia undugu wa OAU, sifa zake zinaendelea kudumu kwa alama zisizofutika kwa namna alivyokuwa nambari moja kupigania ukombozi wa nchi za Kiafrika, vita vyao vikiweka makazi nchini na kwa namna ya pakee, mathalani mataifa ya Kusini mwa Afrika; Msumbiji, Afrika Kusini, Botswana, Southern Rhodesia (Zimbabwe), Namibia na Angola,'

Ni historia inayorejesha viongozi kama Rais Nelson Mandela, nyendo zake za siasa za ukombozi Kusini mwa Afrika, ana nyayo zake nchini, hata historia kiatu chake kwa wenyeji Mama Vicky Nsilo Swai- mjini Moshi) na Samora Machel na ndugu zake waliishi miaka nenda rudi, nchini Tanzania.

**AZIMIO LA ARUSHA**

Mwaka 1967, Tanzania ikiwa ya siasa ya chama kimoja, muumini 'kindakindaki' wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, kiongozi mkuu wa kiserikali na kichama-TANU, Mwalimu Nyerere, alikuja na ubunifu wa kichama uliotekelezwa kiserikali, Azimio la Arusha.

Ni uamuzi uliopewa ufafanuzi kwamba, "ni tamko rasmi la chama kuhusu namna nchi itakavyoendeshwa kupitia Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea".

Maudhui ya tamko hilo yalibeba sura kuu tano ambazo ni makusudio yanayosomeka: "Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, tumepuuzwa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka mapinduzi, mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena, tusinyonywe tena na tusipuuzwe tena".

Mtikisiko wa utekelezaji wake kwa kiasi kikubwa uliangukia utaifishaji wa mali binafsi, za kigeni na ndani ya nchi na kukazaliwa tafsiri mpya za kina, namna uchumi wa taifa utakavyoendeshwa, katika sura kuu ya milki ya pamoja kupitia serikali.

Ni mfumo uliodumu hadi mwaka 1985, yalipotokea mabadiliko makubwa ya mwenendo wa uendeshaji wa uchumi kitaifa, ulioingia katika mfumo huria, msingi wake mkuu ulianzia katika mageuzi ya kiuchumi na siasa kimataifa, sera huria zikichukua nafasi, na kisiasa nchini.

Pia, katika siasa za ndani ya nchi, ilikuwa kipindi Mwalimu Nyerere anastaafu baada ya kutumikia nafasi hiyo kwa miaka 24, na nafasi hiyo alirithiwa na Ali Hassan Mwinyi.

**MWALIMU NA KILIMO**

Ni vigumu sana kumtofautisha Mwalimu Nyerere na kilimo, kwa matendo na vitendo, hata maisha ya kujifunza alikuwa 'bwana shamba' wa aina yake. Alitetea kilimo kwenye hotuba zake, mipango ya serikali na hata alipostaafu, aliamua kuwa mkulima.

Hicho kilichangia sana, miaka michache baada ya uhuru katika zama hizo za miaka ya 1960, Tanzania ilikuwa kinara duniani katika uzalishaji wa katani na pamba, na akawaimarisha wakulima kwa kuwapigania na kuwapa nguvu ya kiuchumi na maendeleo kwa ujumla, kupitia vyama vya ushirika alivyowaanzishia.

Ni aina ya ubunifu alioamua kuwekeza kwa kina kitaalam katika vyuo vya utafiti na vya kilimo ilivyokuwapo na alivyovianzisha, kuongeza kasi ya uzalishaji shambani. Hapo kuna orodha pana, mathalani Naliendele Mtwara kuongeza thamani ya korosho, Ukiliguru Mwanza (pamba), Ilonga Kilosa na Uyole Mbeya, pasipo kusahau tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mjini Morogoro kwa ajili ya kilimo na Ushirika Moshi.

Zama hizo, mabwana shamba na mabwana ushirika walitapakaa kila kijiji kiwe cha ujamaa au kawaida, wakiwawajibikia wakulima ambao wana watoto wao wanaosoma shule zilizoko kijijini.



# TAKUKURU yaokoa bil. 1.4/- za miradi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma katika mwaka fedha 2019/20 imeokoa Sh. Bilioni 1.4 ambazo ni fedha za miradi mbalimbali ya maendeleo, mikopo umiza na vyama vya akiba na mikopo.

Akizungumza na Nipashe jana , Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema fedha hizo zimerejeshwa serikalini kuendelea kufanya kazi katika miradi ya maendeleo ambayo ilifanyiwa ubadhirifu. Pia alisema fedha za vyama vya ushirika na watu wa mikopo umiza zimerejeshwa kwa wahusika.

Mbali na fedha hizo, alisema kipindi hicho imekamilisha uchunguzi majalada 88 na kufungua kesi 44 katika mahakama mbalimbali.

Kibwengo alisema kesi 10 tayari zimesikilizwa mahakamani na kati ya hizo kesi nane Jamhuri imeshinda huku kesi mbili ikishindwa.

Alisema kati ya kesi hizo Jamhuri ilizoshindwa, moja imekata rufani na taratibu zinaendelea mahakama husika.

“Ushindi upo zaidi ya asilimia 80 kwa sababu kesi zilizofunguliwa tumeshinda nane na mbili tulizoshindwa moja tumeikatia rufani ,” alisema Kibwengo.

Kuhusu ukamilishaji wa majalada ya uchunguzi waliofanya, alisema majalada 33 yamefikishwa katika Ofisi ya Mashtaka ya Taifa kwa ajili ya kuombewa kibali kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Hata hivyo, Kibwengo alisisitiza watu kuwa makini na fedha za serikali wanazokabidhiwa kwa ajili ya kutekeleza maendeleo wazifanyie kazi ipasavyo bila kuleta ubadhirifu.

Alisema fedha zinatolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi, hivyo zinapaswa kutumiwa vizuri ili zilete thamani halisi ya fedha.

Alisema TAKUKURU ina jukumu la kufuatilia miradi ya maendeleo iliyoko katika sehemu mbalimbali ili kuhakikisha fedha inayotolewa inatumika kwa ufanisi.

Kutokana na hilo, aliwataka wananchi kutambua kuwa miradi iliyopo sehemu yoyote ni ya kwao, wanapaswa kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo pindi wanapobaini kuna ubadhirifu.



Ofisa kutoka Wizara ya Fedha, Richard Chisimbili (kushoto), akichukua taarifa za Mzee Abdalah Seleman (90), mkazi wa Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma, wakati wa uhakiki wa wastaafu wanaolipwa fedha na hazina ya Serikali kitaifa, lililoanza katika Ofisi ya Halmashauri ya Kongwa juzi hadi Desemba 14, mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Bil. 5/- kukarabati nyumba za TBA

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAKALA wa Majengo Tanzania (TBA), unatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni tano kukarabati nyumba 2,311 nchini jkote.

Kufuatia ukarabati huo, TBA imewataka wapangaji wake kulipa haraka fedha za pango wanazodaiwa ili kusaidia kukamilisha ukarabati huo unaoendelea sasa..

Mkurugenzi wa Milki wa TBA, Said Mndeme, aliyasema hayo jana alipokuwa akikagua ukarabati wa nyumba za wakala katika eneo la Area D jijini hapa.

Alisema ukarabati huo unatarajiwa kukamilika katika kipindi kisichozidi wiki nane huku akisema ni miaka 30 imepita tangu kufanyika ukarabati wa aina hiyo.

“Napenda kutoa rai kwa wapangaji wote nchini kulipa kodi zao kwa haraka ili tuendane na kasi ya kukarabati wa nyumba hizi maana ukarabati unahitaji fedha na hizo fedha ni hizo kodi za pango wanazopaswa kulipa,” alisema.

Aidha, alisema wameanza ukarabati wa nyumba na majengo ya viongozi katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma.

Hata hivyo, alisema ukarabati huo katika eneo la Area D wameanza kwa kukarabati paa na kuboresha sehemu ambazo zinavuja maji.

“Ukarabati huu wa nyumba pamoja na majengo ya viongozi unatarajiwa kukamilika Februari mwakani na nyumba zote zitakuwa katika mazingira bora,”alisema.

Naye Msimamizi wa Mradi wa Ukarabati eneo la Area D, Dismas Liwenga, alisema wamejipanga kukamilisha ukarabati huo kwa wakati ndani ya wiki nane ambapo unajumuisha kukarabati mifumo ya majitaka.

# DED ataka umakini kubaini kaya maskini

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omary Mkulo, amewataka wasimamizi wa uhakiki wa wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini nchini kuhakiki kwa umakini na uaminifu ili fedha hizo ziwafikie wenye sifa.

Dk. M kulo alisema hayo hiyo jana kwenye mafunzo ya siku moja kwa wasimamizi wa awamu ya pili ya kuhakiki kaya maskini wilayani humo, mpango unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Aliwataka wasimamizi hao kutenda haki katika kuzibaini kaya hizo zitakazostahili kuingia kwenye mpango huo wa serikali wenye nia ya kuzikomboa kiuchumi.

“Ndugu zangu uhakiki huu ni muhimu sana kwa sababu tukienda kinyume tunaweza kuingiza watu wasio na sifa na wakiingia watu ambao hawana sifa tafsiri yake ni kwamba wataendelea kupokea fedha za serikali ambazo zingewasidia watu masikini,” alisema.

“Ukiiacha kaya maskini halafu ukaingiza kaya yenye uwezo , yaani hata kwa Mungu utakuwa hujatenda haki kwa sababu tutakuwa tumwemwacha yule ambaye anastahili kuwepo kwenye mpango huo,” aliongeza. Aidha, aliwataka kusimamia kwa makini na kuziondoa kaya ambazo zimekosa sifa ya kuendelea kupokea ruzuku hiyo.

Naye Ofisa Ufuatiliaji na Ushauri wa TASAF wilayani hapa, Sopi Samuel, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watoa huduma kabla ya kuanza kuingia kwenye uhakiki ambao ulianza jana hadi Desemba 11, mwaka huu.

Samuel alisema uhakiki huo unaendeshwa nchi nzima kwa mikoa iliyobaki ya Tanzania Bara na Visiwani na kwamba tayari mikoa 12 ya Tanzania Bara imekamilisha kazi hiyo.

Aliitaja mikoa iliyokamilisha kazi hiyo kuwa ni Mwanza, Kagera, Rukwa, Katavi, Simiyu, Shinyanga, Songwe, Mbeya, Mara, Kigoma, Tabora na Geita. Alibanisha kuwa awamu ya kwanza ya uhakiki ilifanyika kuanzia Julai mpaka Septemba, mwaka huu, na sababu ya serikali kurudia uhakiki kwa awamu ya pili ni kutoa fursa kwa kaya zilizoachwa kutokana na kutokuwapo wakati wa zoezi awamu ya kwanza.

Alisema wasimamizi 20 walipata mafunzo hayo na watashiriki kurudia uhakiki walengwa wa mpango huo kwenye vijiji 43 vya wilaya ya hiyo.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Kongwa , Unambwe Erasto, alisema kaya maskini 6,905 zilihakikiwa na kwamba kaya 6,656 kati ya hizo zilikuwa na sifa ya kuendelea kupata ruzuku hiyo. Erasto alisema baada ya kuhakiki, uhawilishaji wa fedha ulifanyika na kaya hizo zimepokea Sh. milioni 466.3 kuanzia Septemba hadi Desemba, mwaka huu.







Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakila kiapo cha uongozi, wakiongozwa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya, Aliko Mwandumbya (hayupo pichani), wilayani humo, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Ataka mazingira wezeshi shule zote

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewaagiza maofisa elimu, kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwenye shule za msingi na sekondari kufanikisha upatikanaji elimu jumuishi isiyowatenga wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Aliyasema hayo kwenye maadhimisho ya Siku ya Walemavu Duniani iliyofanyika katika viwanja vya shule ya wenye ulemavu inayomilikiwa na Shirika la Child Support Tanzania (CST).

Katika hotuba ya Chalamila aliyowasilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Wiliam Ntinika, alisema hakuna haja ya kuwatenganisha watoto wenye mahitaji maalum na wasio nayo kwa vile wote wanahitaji kujifunza kwa pamoja.

Alitoa agizo hilo baada ya kushuhudia namna Shirika la CST lilivyofanikiwa kutoa elimu jumuisha kwa watoto bila ya kuwatenganisha likitumia mbinu za ubunifu ikiwamo ya vifaa vya kuwavuta wenye mahitaji maalum wazingatie wakati mwalimu akifundisha. Alisema maofisa elimu katika mkoa wa Mbeya wanapaswa kuiga mfano na kujifunza kutoka CST na kuachana na mfumo wa kuwabagua wanafunzi wenye mahitaji maalum shuleni kwa kuwatenga kwenye shule zao au madarasa maalum.

Katika hatua nyingine Chalamila aliziagiza taasisi za umma na binafsi katika mkoa wa Mbeya kutoa nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu kama sheria inavyoelekeza.

Aliongeza kuwa ofisini kwake wapo watumishi wenye ulemavu na wanafanya kazi kwa bidii ukilinganisha na wengine, huku akilipongeza shirika hilo kwa kuwa mfano wa kuwaajiri watumishi wake wenye mahitaji maalum.

Mkurugenzi wa Shirika la CST, Noelah Msuya, aliiomba serikali kufikiria kuanza kutoa elimu ya lugha ya alama kwa wanafunzi wa kuanzia darasa la awali ili miaka ijayo taifa lisiwe na uhaba wa walimu wa lugha hiyo.

"Jamii bado ina uelewa duni na mitazamo hasi kwa watu wenye ulemavu na jamii jumuishi nadhani ni kitu ambacho tunapaswa kuendelea kukipigia mbinja ili watu wengi zaidi waelewe, lakini serikali itusaidie kuihamasisha jamii ishiriki kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki zao za msingi katika jamii," alisema Chalamila.

# DC ataka madarasa 65 kabla ya Januari

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, ameagiza viongozi pamoja na madiwani kuwahamasisha wananchi kujenga vyumba 65 vya madarasa kabla ya Januari mwakani.

Mfune alitoa kauli hiyo jana wakati wa kuwaapisha madiwani wa Halmashauri ya Mbarali na kuongeza kuwa kuna uhaba wa vyumba vya madarasa 65 na kuagiza ujenzi kuanza mara moja, wanafunzi wa kidato cha kwanza waanze masomo kwa wakati.

"Nawapongeza madiwani kwa kupata nafasi ya kuwawakilisha wananchi, matarajio yangu ni kwamba mtaisaidia halmashauri yetu katika masuala mbalimbali ya maendeleo likiwamo hili la ujenzi wa vyumba vya madarasa," alisema Mfune. Madiwani na watendaji wa kata na vijiji wana jukumu la kuhamasisha wananchi kujitoa kwa hali na mali kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo, aliagiza.

Mkurugenzi wa Halmashauri, Kivuma Msangi, alisema moja ya mikakati katika kuhakikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa unakamilika ni pamoja kuhimiza umoja na mshikamano baina ya watendaji na madiwani ili kuleta maendeleo.

Alisema vyumba 40 havijajengwa na vyumba 25 viko katika hatua mbalimbali za ujenzi hivyo akahamasisha kuongeza kasi ili kuepuka usumbufu ifikapo Januari wakati watoto wa kidato cha kwanza wakitakiwa kuanza masomo.

Aidha, Kivuma aliwasisitiza madiwani hao kushughulikia kero mbalimbali za wananchi bila kujali itikadi za kisiasa kwa kuhakikisha wanakuwa ni viongozi kwenye kushirikisha wengine katika ngazi za maamuzi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Tamim Lubandamo, aliyeshinda kiti hicho kwa kura 26 kati ya 27 zilizopigwa na madiwani aliwaomba kuachana na chuki pamoja na visasi.

Alihimiza kuchapa kazi na kuachana na chuki ambazo zilijitokeza wakati wa uchaguzi na kwamba yeyote atakayejaribu kutia doa ndani ya wilaya hiyo atachukulia hatua.

Alimhakikishia Mkuu wa Wilaya kwamba ujenzi wa vyumba vya madarasa utakamilika kabla ya Januari, huku akiwaomba wadau kuongeza ushirikiana na serikali kuongeza bajeti ili kukamilisha ujenzi huo.

Alisema watakwenda kuwahamasisha wananchi kuchangia ujenzi huo katika namna ambayo haitawaumiza kutokana na kwamba hivi sasa ni msimu wa kilimo.

## Ashikiliwa kwa madai ya kuiba dizeli lita 140

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWANAKIJIJI cha Isanura kilichoko Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Enock Gongo (37), anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za wizi wa lita 140 za dizeli.

Kamanda wa Polisi mkoani Mbeya, Urich Matei, alisema katika taarifa yake kuwa alinaswa juzi Jumatatu, saa 12 jioni huko Isinura, baada ya kufanya msako.

Matei alisema mtuhumiwa alikutwa na mafuta hayo yaliyohifadhiwa kwenye madumu saba ya lita 20 na katika mahojiano alikiri kuyaiba Novemba 29 mwaka huu, saa 11 alfajiri katika kijiji cha Manienga.

Alisema mali hiyo ilikuwa ya Trespod Sambi (43) daktari na anayeishi Ihanga, Kata ya Rujewa na kwamba mtuhumiwa atafikishwa mahakamani, wakati wowote.

Katika hatua nyingine polisi inamtafuta dereva wa gari namba T.564 DFE aina ya Toyota Mark 11 ambaye hajafahamika, anayetuhumiwa kumuua dereva wa pikipiki.

Alisababisha ajali hiyo akitokea Mbeya kwenda Mbarali wakati alipomgonga dereva wa bodaboda namba T.165 DRC na kusababisha kifo chake ambaye naye hajafahamika.

"Tukio hilo lilitokea Jumatatu Desemba 7, saa 3:00 usiku eneo la Imezu, wilayani Mbeya katika barabara ya Mbeya-Njombe, ambapo chanzo cha ajali ni mwendo kasi wa dereva wa gari," alisema Kamanda Matei na kwamba marehemu, amehifadhiwa kituo cha afya Inyala kwa uchunguzi.



# Makamu Rais anusa rushwa mamlaka ya maji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), imetakiwa kufanya uchunguzi wa pampu saba za kusukumia maji zilizonunuliwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) hivi karibuni.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alitoa agizo hilo jana na kutaka uchunguzi huo ukamilike ndani ya wiki moja.

Aliyasema hayo alipofanya ziara ya kushtukiza katika makao makuu ya ZAWA Kinazini mjini Zanzibar. Hemed alisema amefikia uamuzi wa kutoa agizo hilo ili serikali ipate kujiridhisha kama hakuna dalili yoyote ya harufu ya rushwa kwenye ununuzi hayo. Hemed alisema serikali haitavumilia kuona mamlaka hiyo ya maji ambayo ni taasisi muhimu inayogusa maisha ya wananchi inazungukwa na uzembe unaoweza kusababisha athari na kupungua kwa mapato ya serikali. Alisema kuanzia sasa, mtumishi yeyote wa taasisi za umma anayeharibu na kushindwa kuwajibika katika eneo lake la kazi, huo utakuwa mwisho wa utumishi wake. Hemed aliutaka uongozi wa mamlaka hiyo kujisafisha kwa kuondoa hitilafu za migogoro ya uongozi ndani ya mwezi mmoja vinginevyo serikali itasafisha safu hiyo ya uongozi kwa maslahi ya umma.

Alisema wahandisi wa taasisi hiyo wanapaswa kurekebisha miundombinu sambamba na kuweka utaratibu utakaoharakisha watendaji kuwajibika ipasavyo ili kuwapa fursa wananchi kupata huduma za maji safi na salama muda wote.

Makamu wa Rais alisema uwajibikaji kwa watendaji wa mamlaka hiyo uko chini kutokana na tabia ya muhali inayochukua nafasi kubwa na matokeo yake hata makusanyo ya mapato yatokanayo na huduma za maji hayafikii lengo lililokusudiwa.

Pia aliwataka wafanyakazi kuendelea kufuatilia mwenendo wa upatikanaji wa huduma za maji safi na salama katika maeneo yote ya Unguja na Pemba ili kuondoa au kupunguza kabisa malalamiko ya yanayosikika kila wakati kwenye vyombo vya habari kuhusu huduma hiyo.

Alisema suala hilo ni vyema likaenda sambamba kwa watendaji hao kuhakikisha kwamba wananchi na taasisi zote zinazotumia huduma hiyo zinawajibika kulipa huduma hiyo ili taasisi hiyo kujiendesha badala ya kuendelea kupeleka maombi ya kupatiwa fedha serikali kuu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA, Mussa Ramadhan Haji, alisema hali ya upatikanaji wa huduma za maji safi na salama ndani ya Unguja na Pemba kwa sasa imefikia asilimia 80 kulingana na matumizi yaliyopo.

Alisema wakati mwingine hali hiyo hushuka hadi asilimia 75 kutokana na baadhi ya visima vya maji kukumbwa na hitilafu za umeme lakini pia baadhi ya mashine za kusukumia maji huharibika kutokana na kutumika kwa muda mrefu hasa katika baadhi ya maeneo yasiyo na matangi ya kuhifadhia maji.

Mussa alisema katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na huduma za usambazaji maji, wataalamu wa mamlaka hiyo wameanza kufanya utafiti wakianzia eneo la Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja ili kubaini kasoro zinazochangia tatizo hilo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akizungumza alipofanya ziara ya kushtukiza katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi mjini Zanzibar jana. Aliagiza uchunguzi ufanyike dhidi ya mashine saba za kusukuma maji zilizonunuliwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). **PICHA: OMPR – ZNZ**

# RC mstaafu ampa neno mrithi wake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Vuai Mwinyi Muhammed, amemwomba Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Mohammed Mahmoud, kusimamia maeneo yote ya ardhi ya serikali yaliyotengwa kwa ajili ya uekezaji ili yasivamiwe na wananchi

Vuai aliyasema hayo jana wakati akizungumza na watendaji mbalimbali katika mkoa huo ikiwamo kamati ya ulinzi na usalama katika hafla ya makabidhiano ya ofisi huko Mkokotoni.

Alisema serikali imeyatenga baadhi ya maeneo likiwemo la Bumbwini kwa ajili ya uwekezaji wa gesi na mafuta Matemwe ambalo linatarajia kujengwa hoteli kubwa ya kitalii itakayokuwa na hadhi kubwa duniani.

Vuai alisema endapo maeneo hayo yatasimamiwa ipasavyo, yatasaidia kwa kiasi kikubwa kukamilika kwa miradi hiyo ambayo itazalisha fursa za ajira kwa wanachi.

Akizungumzia maendeleo katika kipindi chake cha uongozi wake, alisema amepeleka maendeleo katika vijiji vya Mbuyu Maji, Mlilile na Mgonjoni kwa kupata huduma muhimu za kijamii zikiwamo maji safi, umeme na afya

Licha ya maendeleo hayo, alisema bado kuna tatizo la lami kwa barabara za vijiji hivyo na kuiomba serikali kupeleka huduma hiyo ili kuwaondolea usumbufu wa huduma ya usafiri wananchi wakiwamo kinamama na watoto.

Naye Ayoub aliyataka mabaraza ya miji katika mkoa huo kutafuta maeneo yanayovujisha mapato ili kudhibitiwa pamoja na kuahidi kusimamia miradi yote ya serikali.

Kuhusu elimu, alisema kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu, watashirikiana ili kuinua kiwango cha sekta hiyo katika mkoa huo.

Aliwataka watendaji wote katika mkoa huo kushirikiana na kuweka mipango madhubuti itakayosaidia kupeleka mbele gurudumu la maendeleo na kuahidi kuimarisha ulinzi na usalama ambao utakuza sekta ya utalii.

# Asisitiza walimu kujengewa uwezo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mafunzo ya Ualimu kutoka Wizara ya elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Maimuna Fadhil Abbas, amesema kuna umuhimu wa kupewa taaluma na kuwajengea uwezo walimu katika masuala mbalimbali ili kukuza uelewa na kutoa elimu kwa watoto.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu namna ya kuwafundisha watoto masuala ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi pamoja na stadi za maisha, katika ukumbi wa kituo cha Walimu Kiembe Samaki mjini Unguja.

Maimuna alisema hali hiyo itawasaidia watoto kujitambua kijinsia na kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo za udhalilishaji.

Alisema bado kuna watoto hawajitambui kutokana na wazazi kuwa na aibu ya kuwaficha na kutokuwa karibu nao katika kuwapa stadi za maisha na kujitambua.

Taaluma ya uzazi salama na afya pamoja na virusi vya Ukwi na Ukimwi, alisema inapaswa kutolewa kwa jinsia zote si kwa wanawake pekee na kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kusaidiana katika hali mbalimbali katika mzunguko wa maisha yao.

Aliwataka walimu hao kutumia lugha nzuri katika kuwafundisha watoto juu ya masuala hayo na si kuficha hali ambayo haitawasaidia katika kujua namna ya kujilinda afya zao hasa kipindi wanachoanza kupata ukubwa.

Maimuna alisema wameamua kuwapa mafunzo hayo walimu kutokana na wao kuwa ndio wako karibu na wanafunzi kwa kuwapa ushauri nasaha juu ya dhana nzima ya kujikinga na matatizo mbalimbali yakiwamo ubakaji, udhalilishaji na kujitambua na kuwafanya kuwa huru kuwaambia matatizo mbalimbali yanayowakabili.

Pia alisema walimu wana wajibu mkubwa wa kuwalinda na kuhakikisha wanawapa elimu bora watoto katika mazingira yote wakiwa shuleni na hata nyumbani na kuwazoesha kusema hapana ili kuwakinga na vitendo mbalimbali ikiwemo ya udhalilishaji.

Hata hivyo, alisema walimu bado wanahitaji mafunzo kuhusu masuala ya elimu ya uzazi, hivyo alilishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kuona umuhimu wa kutoa elimu hiyo na kujitolea kufadhili.

Naye Ofisa wa Elimu na Afya kutoka UNESCO Zanzibar, Hasina Salim Bukheti, alisema mafunzo hayo yanafanyika kupitia mradi wa haki za mtoto, maisha ya mtoto na mustakabali mzima wa mtoto na kijana katika afya na elimu.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwasaidia watoto kujengea uwelewa wa afya ya uzazi salama, kuwa imara, kuwapa taarifa sahihi za kijinsia ili kujilinda, kujiamini na kusimamia vizuri haki za msingi na kupata maisha mazuri baadaye.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA KAZI

**Nafasi za kazi ya ualimu Diploma**
**- Kiswahili**
**-Science SST**
**- Kiingereza**
**Mawasiliano:**
**0783 334653**


NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**


Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MUSTAFA HERRY** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 535 CNQ TVS RANGI NYEUSI.** Yeyote atakayaiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: MTW/MTW/RB/831909/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LILIAN AUDIFAS RIMOI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE **NO S0679-0050** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA KIMANDOLU SEKONDARI MWAKA 2015. YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI**
**USR/ RB/S253/2018.**


**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

# JKT yakabidhiwa trekta, mashine ya kufyeka

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), imeikabidhi Kamandi ya Jeshi la Anga, trekta pamoja na mashine maalum ya kufyeka nyasi katika Uwanja wa Ndege wa Ngerengere uliopo mkoani Morogoro.

Mwanasheria Mkuu wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Meja Jenerali, Kaisy Njelekela, akimwakilisha Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Faraji Mnyepe, alisema katika makabidhiano jana kuwa, trekta hilo limegharimu Sh. milioni 48.7 na Mkuu wa Jeshi la JKT, Meja Jenerali, Charles Mbuge ameunga mkono kwa kununua kifaa cha kufyekea kwa Sh. milioni 8.5.

Makabidhiano hayo yalifanyika makao makuu ya JKT, jijini Dar es Salaam.

Katika hotuba yake, Katibu Mkuu alisema, wizara yake inatambua umuhimu wa uwanja huo ambao umekuwa ukisafishwa kwa kufyekwa na askari.

"Trekta hili na mashine hii itasaidia kurahisisha shughuli za usafi katika uwanja huu, nguvu kazi ambayo ilikuwa ikitumika kufyeka itumike sehemu nyingine," alisema.

Pia, aliagiza trekta pamoja na mashine hiyo na vifaa vingine vitunzwe ili vidumu muda mrefu.

"Itakuwa ajabu ndani ya muda mfupi kukuta trekta lipo juu ya mawe, serikali itatushangaa endapo vifaa vinavyonunuliwa kwa gharama kubwa viharibike kwa sababu hatujui ni lini tena tutapata vingine kama hivi," alisema.

Alisema endapo litaharibika ndani ya muda mfupi, watakaowajibika kufyeka kwa mikono ni wao wenyewe.

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Charles Mbuge, alisema trekta hilo ni miongoni mwa 150 ambayo yanauzwa kwa fedha taslimu.

Alisema kupitia mfumo huo wa uuzaji wa fedha taslimu, tayari matrekta 25 kati ya 150 yameshauzwa likiwamo hilo lililokabidhiwa kwa Kamandi ya Jeshi la Anga.

Alisema mfumo huo wa uuzaji unalisaidia jeshi hilo kujitegemea kwa kuzalisha chakula kama serikali ilivyoagiza kupitia Rais John Magufuli ambaye mara kwa mara ameyataka majeshi kujitegemea katika uzalishaji wa chakula.

Brigedia Jenerali, Shabani Mani, akimwakilisha Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, Meja Jenerali George Ingram, alisema, Kamandi hiyo inamiliki vifaa vyenye gharama kubwa na kuahidi kulitunza trekta walilokabidhiwa.

Alisema uwanja wa ndege wa Ngerengere umetengenezwa na kukarabatiwa kwa ubora wa kimataifa na ununuzi wa trekta hilo utasaidia kuutunza kwa ubora unaostahili.



Kamishna wa Fedha anayesimamia Sekta za Maendeleo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamaja (wa pili kushoto), akikabidhi tuzo ya ushindi wa kwanza wa kipengele cha wazalishaji bora katika Uwasilishaji Bora wa Taarifa za Mahesabu za Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) ya mwaka 2019 kwa Mkuu wa Divisheni ya Fedha wa Kampuni ya Tanga Cement Plc, Isaac Lupokela, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wenye ulemavu waonyeshwa ujuzi

**Na Edina Alex, SINGIDA**

WATU wenye ulemavu wametakiwa kutumia fursa ya uwapo wa vyuo vinavyotoa huduma kwa watu hao ili kupata ujuzi utakaowasaidia kujitegemea kiuchumi.

Miongoni mwa vyuo hivyo ni cha ufundi na marekebisho Saba Saba, kilichopo mkoani hapa, ambacho kinatoa huduma za masomo kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

Akizungumza kwenye sherehe ya mahafali ya 43 ya chuo hicho, mwakilishi kutoka kampuni ya uchimbaji madini (Shanta Golding Mining), Elisante Kanuya, aliwataka watu wenye ulemavu kutumia fursa hiyo ili kuondokana na utegemezi.

"Nimeona hapa mnafundishwa mambo mengi, ya umeme, ushonaji na vitu vingine ikiwamo kutengeneza bidhaa mbalimbali, naomba mtumie ujuzi huo mnaoupata kujiajiri ili kujiletea maendeleo," alisema Kanuya.

Aliwataka waliohitimu mafunzo yao kwenda kuwa mfano chanya kwenye jamii na kujiendeleza kupitia ujuzi walioupata kwa kuwa bila kuutumia wataendelea kuwa tegemezi.

"Nawakaribisha nyinyi wahitimu kwa ujuzi wenu Shanta Golding Mining pindi utakapoanza kufanya kazi ili mje mtumie ujuzi wenu kwa manufaa yenu, kampuni na taifa kwa ujumla," alisema.

Aliwaomba wadau mbalimbali kuhakikisha wanaunga mkono juhudi zinazofanywa na uongozi wa chuo kuhakikisha wanaboresha mazingira ya kujifunzia wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kutatua matatizo mbalimbali yanayokikabili chuo hicho.

Mkuu wa chuo hicho, Fatma Malenga wakati akitoa taarifa ya chuo, alisema kilianzishwa mwaka 1977 kikiwa na jina la chuo cha wanawake wasioona na baadaye kuitwa chuo cha ufundi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu.

Alisema lengo la kuanzishwa ilikuwa ni kutoa huduma za marekebisho na kuwawezesha watu wenye ulemavu wapate ajira na kujitegemea kiuchumi.

Malenga alisema kwa sasa chuo hicho kinapokea wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi, viziwi, wenye ulemavu wa viungo, wasioona na wenye tatizo la mtindio wa ubongo kwa jinsia zote na mwaka huu, chuo kilipokea wanachuo 228, pia wanaendelea kupata mafunzo ya fani za ufundi wa umeme wa majumbani, useremala, ushonaji, maandishi ya nukta nundu, kilimo, mapishi na maarifa ya nyumbani, afya ya uzazi na stadi za kazi.

Aliwaomba wadau kukisaidia kuweka uzio kwa ajili ya ulinzi na usalama, ujenzi wa ukumbi wa mikutano, madarasa na karakana.

# RC aipa tano IRUWASA

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) kwa kuendelea kufanya vizuri na kupata tuzo za utoaji huduma bora za maji.

Hapi alitoa pongezi hizo jana, wakati wa mkutano wa wadau wa IRUWASA uliofanyika kwenye ukumbi wa Siasa ni Kilimo, mjini hapa.

Alisema kwa vipindi tofauti, IRUWASA imeendelea kushinda tuzo kwa nafasi ya kwanza na ya pili jambo ambalo ni heshima kubwa kwa mamlaka hiyo.

Kwa mujibu wa Hapi, jitihada kubwa zinazofanywa na mamlaka hiyo chini ya Mkurugenzi Mtendaji, Gilbert Kayanga, na watumishi wote ni chachu ya tuzo hizo na inatokana na kazi kubwa wanayoifanya kusogeza huduma kwa wananchi wa Iringa .

Pamoja na pongezi hizo, hapi aliwataka watumishi wa IRUWASA kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kuwa na matumizi mazuri ya maji ili kuepuka malalamiko ya kuletewa bili kubwa za maji.

"Lazima kuendelea kuwapa elimu wananchi juu ya matumizi ya maji. Wako baadhi ya wanawake wakiingia bafuni kuoga wanatumia maji vibaya, unakuta mtu anapooga anajipaka sabuni kuanzia mguuni hadi kichwani huku maji yakiendelea kumwagika. Tambua hizo ni pesa pia," alisema Hapi

Alisema wananchi lazima waendelee kupewa elimu juu ya matumizi bora ya maji ili badala ya kutumia maji mengi, wajifunze kutumia maji kidogo zaidi na ikiwezekana mita za LUKU kuendelea kusambazwa zaidi.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa alionya tabia za baadhi ya watu wanaohujumu miundombinu ya maji na kuwa watu hao hawatavumiliwa kamwe.

"Hatuwezi kuendelea kuwa na huduma ya uhakika na endelevu ya majisafi bila wote kushiriki katika kutunza na kulinda vyanzo vya maji na kulinda miundombinu ya maji," alisema.

Alisema vyanzo vya maji visipolindwa na kutunzwa, maji yataisha na ubora wake utaathirika na matokeo yake mahangaiko ya kutafuta maji kwa wananchi yataongezeka na hata afya zao zitaathirika.

"Sote tu mashahidi namna IRUWASA ambavyo imekuwa ikitoa huduma kwa viwango vya hali ya juu. Utoaji wa huduma ya majisafi umefikia asilimia 96 ya mji wa Iringa na maji yanapatikana kwa wananchi kwa takribani saa 24.

IRUWASA kwa sasa imeanza kutoa huduma nje ya mipaka ya Manispaa ya Iringa ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa katika kata za Luhota, Mseke, Kalenga, Kiwele, Kisinga na Kihorogota. Pia kwa sasa IRUWASA inahudumia miji ya Kilolo na Ilula.

## HABARI MICHEZO

# MBAPPE NENDA REAL MADRID - SUKER



**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, ana ubora na anafaa kuwachezea mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid, kwa mujibu wa straika wa zamani wa 'Los Blancos' hao, Davor Suker.

Mbappe amekuwa akipewa nafasi ya kujiunga na Madrid wakati akiingia katika miezi yake 18 ya mwisho kwa PSG, huku mabingwa wa Ligi Kuu England, Liverpool pia wakihusishwa naye.

Mabingwa wa Ligue 1, PSG wanaangalia uwezekano wa kuongeza mkataba na Mbappe baada ya msimu wa 2021-22.

Suker ambaye kwa sasa ni Rais wa Shirikisho la Soka la Croatia (HNS), baada ya kutumia miaka mitatu akicheza pale Madrid, ambako alishinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya mwaka 1996 na 1999 - ameelezea uwezekano wa Mbappe kwenda kule Santiago Bernabeu.

"Kuna fedha nyingi kwenye soka hivi sasa, lakini kama hakuna njaa mchezaji kamwe hatafanikiwa," alisema Suker mwenye umri wa miaka 52 akiiambia beIN Sports France.

"Unatakiwa kuangalia mchezaji ambaye ana njaa na nafikiri (Kylian) Mbappe ana kitu kama hicho na anahitajika kuichezea Real Madrid.

"Mimi si mwakilishi wake na naweza tu kuzungumzia kuhusu mchezaji ambaye ananivutia."



# LOW

## AWAKAZIA MULLER, BOATENG NA HUMMELS

**MUNICH, Ujerumani**

JOACHIM Low atafanya kile anachohisi ni bora kwa Ujerumani kupata mafanikio katika michuano ya Euro 2020 wakati linapokuja suala la maamuzi ya kuwarudisha kikosini Thomas Muller, Jerome na Mats Hummels.

Wachezaji wote watatu waliondolewa kwenye kikosi hicho cha timu ya taifa na Low Machi mwaka 2019, wakati alipokuwa anajenga kikosi hicho cha Ujerumani baada ya kuwa na matokeo mabaya kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, wakiwa wametolewa hatua ya makundi kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1938.

Kiungo mshambuliaji, Muller (mechi 100), pamoja na walinzi Boateng (mechi 76) na Hummels (mechi 70), kwa pamoja wakiwa wamecheza jumla ya mechi 246 na wote walikuwa kwenye kikosi kilichotwaa Kombe la Dunia mwaka 2014, lakini sasa wote wana umri wa miaka 30.

Low mwezi uliopita alisema angependa kusimamia kile anachokiamini na hayupo tayari kumuita yeyote kati yao akisema "hakuna kilichobadilika" kuhusu mawazo yake, ingawa Muller anafurahia kiwango bora pale Bayern Munich tangu atemwe.

Hata hivyo, maamuzi ya Low yamekuwa yakikosolewa sana na baada ya kichapo cha mabao 6-0 kutoka kwa Hispania, kipigo kikubwa zaidi kwa Ujerumani tangu ilipopoteza dhidi ya Austria kwa idadi kama hiyo ya mabao kwenye mchezo wa kirafiki mwaka 1931.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 60, wiki iliyopita aliungwa mkono na Chama cha Soka cha Ujerumani (DFB), na atabaki na kikosi hicho hadi angalau baada ya Euro 2020 inayofanyika mwakani, na sasa ameonekana kubadili msimamo wake.

"Baada ya mwaka 2018, tuliona kwamba hatukupata mafanikio na tuliamua kufanya mabadiliko," alisema. "Ni muhimu kuwapa nafasi wachezaji vijana ili wajiimarishe.

Alipoulizwa kama yupo tayari kuwaita tena kikosini nyota wa Bayern, Muller na Boateng, au mlinzi wa kati wa Borussia Dortmund, Hummels, Low alijibu: "Hapana, sijaamua."

# ENGLAND KUIVAA POLAND KUFUZU KOMBE LA DUNIA 2022



**NYON, Uswisi**

ENGLAND itakutana na Robert Lewandowski na Poland kwenye michuano ya kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar.

Kikosi hicho cha kocha, Gareth Southgate kimepangwa Kundi I, pia pamoja na Hungary, Albania, Andorra na San Marino.

Mabingwa wa Dunia Ufaransa wapo Kundi D pamoja na Ukraine, Finland, Bosnia-Herzegovina na Kazakhstan.

Uholanzi wapo Kundi G, ambalo lina Uturuki, Norway, Montenegro, Latvia na Gibraltar.

Croatia, ambao walifika fainali michuano iliyopita, wapo Kundi H pamoja na Slovakia, Russia, Slovenia, Cyprus na Malta.

Hispania itawakabili Sweden, Ugiriki, Georgia na Kosovo kwenye Kundi B, huku Ureno ikiwa Kundi A pamoja na Serbia, Ireland, Luxembourg na Azerbaijan.

Mechi hizo zitaanza kupigwa kati ya Machi na Novemba mwakani.




# KOEMAN

## ATAKA NEYMAR AKACHEZE TENA NA MESSI

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, anaamini kuwa Barcelona itafanya kitu kuona msimu ujao Lionel Messi anacheza tena na Neymar ndani ya Camp Nou.

Hii ni baada ya hivi karibuni, Neymar kutamka wazi kuwa msimu ujao anataka kucheza tena na Messi ingawa haijaelezwa wapi kama ni PSG au Barcelona.

Neymar aliondoka Barcelona mwaka 2017 na kutua PSG. Alicheza na Messi ndani ya Barcelona kuanzia 2013, tangu msimu uliopita, staa huyo amekuwa akihusishwa kurejea viunga vya Camp Nou.

Nyota Messi mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, ambapo awali naye alikuwa anahitaji kusepa ndani ya kikosi hicho.

"Kila mmoja anafahamu suala la Messi, mtu pekee anayeweza kuamua hatima yake kwa sasa ni yeye mwenyewe.

"Klabu inapambana kuona inakuwa na wachezaji bora, nataka kuona Messi anacheza hapa na mchezaji bora (Neymar) ndani ya Camp Nou itakuwa vizuri zaidi," amesema Koeman.

## MOURINHO ATETEA MFUMO TOTTENHAM

**LONDON, England**



KOCHA Mkuu wa Tottenham, Jose Mourinho, amesema mfumo wake anaoutumia wa mashambulizi ya kushtukiza kwake ni bora kwa kuwa unampatia matokeo.

Mounrinho alikiongoza kikosi chake Jumapili kushinda mabao 2-0 dhidi ya Arsenal kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, ambapo umiliki wa mpira kwa timu yake ulikuwa 30, huku Arsenal wakiwa na 70.

Mourinho alishuhudia mabao hayo yakifungwa na Son Heung-min na Harry Kane, hivyo kuifanya timu yake kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 24 baada ya kucheza mechi 11 huku Arsenal ikiwa nafasi ya 15 na pointi 13.

Pia nahodha Kane amesema timu inafurahi kucheza katika mfumo wowote lengo lao ni kuona wanapata matokeo ndani ya uwanja jambo ambalo linawafanya wacheze bila presha ndani ya dakika 90, huku wakifanya mashambulizi ya kushtukiza.

Mourinho alisema: "Unapozungumzia habari za umiliki wa mpira hiyo ni falsafa ya kwenye mpira, lakini kwangu mimi naona matokeo ni muhimu zaidi. Hakuna hata mmoja ambaye amewahi kuona nimepoteza mchezo ila nimekuwa na umiliki mkubwa wa mpira.

"Jambo la msingi ni kile ambacho unakifanya na mpira ndani ya uwanja hakuna jambo lingine zaidi ya ushindi, wachezaji wangu wanapenda na wanafurahi.

"Nakumbuka wakati watu wanasema kwamba uwezo wangu umekwisha ila niliweza kutwaa mataji matatu ndani ya Manchester United, nilishinda Super Cup na Ligi ya Europa, sasa wananiambia nimechuja hebu fikiria wapo wengine hawana kabisa haya mataji sasa sijui itakuaje," amesema.



## BALOTELLI ASAJILIWA MONZA

**ROMEO, Italia**

MARIO Balotelli amesaini mkataba na klabu ya Monza ya Serie B (Daraja la Pili) kwa kipindi cha msimu huu kilichobaki.

Straika huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 30, amekuwa mchezaji huru tangu kusitishwa kwa mkataba wake na Brescia ambao walishuka daraja kutoka Serie A msimu uliopita.

Balotelli amekuwa akifanya mazoezi na timu ya Serie D, Franciacorta ili kujiweka fiti wakati akihusishwa na kujiunga na klabu ya Barnsley ya Ligi Daraja la Kwanza England.

Monza kwa sasa inamilikiwa na Silvio Berlusconi (Waziri Mkuu wa zamani wa Italia), ambaye awali alikuwa mmiliki wa AC Milan kati ya mwaka 1986 hadi 2017, ambako Balotelli pia alicheza kwa misimu miwili.

Balotelli alianza kucheza soka akiwa na Lumezzane na pia aliwachezea wapinzani wa jiji moja wa Milan, Inter Milan pamoja na Manchester City, Liverpool, Nice na Marseille.

Taarifa ya Monza, ambao wapo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Serie B, ilisema: "Mario Balotelli amekuja kuiimarisha Monza na amesaini mkataba hadi Juni 30, mwaka 2021.


"Balotelli ni mmoja wa wachezaji saba pekee ambao kuanzia Januari Mosi, 2000, amefunga mabao angalau 20 katika ligi tatu kubwa kati ya tano kubwa za Ulaya. Karibu Mario!"

Balotelli ameifungia Italia mabao 14 na alicheza mechi yake ya mwisho ya 36 ya kimataifa dhidi ya Poland Julai mwaka 2018.

Amepewa jezi namba 45 pale Monza na anaweza kuanza kucheza mechi yake ya kwanza Serie B dhidi ya Venezia, Ijumaa.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA MUDA WAKE UTD UMEISHA - RAIOLA

●●●Hana furaha tena United, anahitaji timu mpya kubadilisha hali ya hewa, na hana uwezo wa...

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba anaweza kurudi kwa mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus kwani hana furaha pale Manchester United, kwa mujibu wa wakala wake, Mino Raiola.

Mwakilishi huyo wa Pogba, Raiola amesema kiungo huyo nyota muda wake pale United umefikia "mwisho" wakati akizungumza kwenye mahojiano na Tuttosport kuhusu uvumi wa nyota huyo kuondoka pale Old Trafford hivi karibuni.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa - ambaye alifunga kwenye mchezo wa Ligi Kuu England Jumamosi wakati wakishinda 3-1 dhidi ya West Ham - mara kwa mara amekuwa akihusishwa na klabu yake ya zamani Juve na mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid, huku Pogba akielezea uhamisho wake wa kwenda kule Santiago Bernabeu kama "ndoto".

Pogba aliondoka United kwenda kwa miamba wa Serie A, Juve mwaka 2012 baada ya mkataba wake kumalizika na akajiunga tena na 'Mashetani Wekundu' hao mwaka 2016 ambapo aliweka rekodi ya dunia kwa ada yake ya pauni milioni 89.

Katika ukurasa wa mbele wa gazeti la Tuttosport la Jumanne, ambako kumechapishwa mahojiano yote, Raiola amenukuliwa akisema: "Ndio, Paul Pogba anaweza kurudi Juventus.

"Hana furaha pale Manchester United."

Kauli hiyo ya Raiola imekuja wakati United ilikuwa ikijiandaa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya RB Leipzig jana Jumanne ambao ni wa mwisho kwa Kundi H.

"Paul hana furaha na Man United na hana uwezo tena wa kujielezea yeye mwenyewe namna mambo yanavyotakiwa kuwa kama ambavyo alitarajia," alisema Raiola.

"Paul anahitaji timu mpya, kubadilisha hali ya hewa.

"Yupo na mkataba wake unamalizika miezi 18 ijayo, mwaka 2022."

Pogba ameichezea United mechi 13 katika mashindano yote msimu huu, akifunga mabao mawili.

## KWA UFUPI

**OZIL KUTUA FANERBAHCE**

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, ana uhakika wa asilimia 90 atajiunga na Fenerbahce mwezi ujao, kwa mujibu wa mmoja wa wajumbe wa bodi ya klabu hiyo ya Uturuki. ***(Sport Digitale, via Mirror)***

**LINGARD KUONDOKA UNITED**

WAWAKILISHI wa Jesse Lingard wanapitia ofa za mkopo kwa kiungo huyo wa Manchester United na England kwa Januari, na Real Sociedad ni moja ya klabu ambayo wamefanya nayo mazungumzo ya awali kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Sky Sports)***

**LAMPARD AMBANIA KEPA**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amesema hana shinikizo la kumuuza mlinda mlango wa Hispania, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 26, ambaye thamani yake ni pauni milioni 71. ***(Evening Standard)***

**UNITED YAMTAKA VAZQUEZ**

MANCHESTER United inaweza kumgeukia mlinzi wa pembeni wa Real Madrid ya Hispania, Lucas Vazquez mwenye umri wa miaka 29, wakati wanatafuta mshindani wa Aaron Wan-Bissaka mwenye miaka 23. ***(Defensa Central)***

**ROMERO KURUHUSIWA KUSEPA**

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumruhusu mlinda mlango wake raia wa Argentina, Sergio Romero kuondoka mwezi ujao na watamuuza ikiwa dau la pauni milioni mbili litafikiwa. ***(Football Insider)***

**HULK SASA KUTUA EPL**

MSHAMBULIAJI wa Brazili, Hulk mwenye umri wa miaka 34, ameondoka klabu ya Shanghai SIPG na amehusishwa na taarifa za kuhamia Ligi Kuu England kwa uhamisho huru. ***(Sun)***

**KASSIE LULU SPURS, ARSENAL**

TOTTENHAM Horspur na Arsenal zinamwania kiungo wa kati wa AC Milan na raia wa Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 23, ambaye ana thamani ya karibu pauni milioni 45 na ambaye mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika Juni 2022. ***(Calciomercato)***

**FABINHO KUTETA NA LIVERPOOL**

LIVERPOOL ina matumaini ya kuanza mazungumzo na kiungo mkabaji, Fabinho mwenye umri wa miaka 27, kuhusu mkataba mpya hivi karibuni.***(Guardian)***

**WILLEMS AIKATALIA FRANKFURT**

JETRO Willems amekataa ofa ya mkataba mpya katika klabu ya Eintracht Frankfurt, hatua inayotoa fursa kwa Newcastle United kumsajili mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Chronicle)***

**LAZAAR KUONDOKA NEWCASTLE**

MLINZI wa kushoto wa Morocco, Achraf Lazaar mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuondoka Newcastle United katika dirisha la Januari, huku mkataba wa mchezaji huyo ukifikia mwisho kipindi kijacho cha majira ya joto. ***(Passione Inter, via Chronicle)***

**GILMOUR HAJUI HATIMA**

KIUNGO wa Chelsea na Scotland, Billy Gilmour mwenye umri wa miaka 19, amesema hajui "majaliwa yake yaliko" klabuni hapo baada ya kurudi kutoka chumba cha majeruhi na huku usajili mpya uliofanywa na Blues hao ukitisha. ***(Star)***

HABARI MICHEZO

# LWANDAMINA AONYESHWA PAKUANZIA AZAM IKISHIKWA

Na Saada Akida

HUKU kinara wao wa mabao, Price Dube, akiendelea kuwa nje akiuguza majeraha ya bega aliyoyapata, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati amesema wana kazi ngumu ya kuiimarisha safu ya ushambulaiji kwa kuipa mbinu sahihi, ili kuweza kutumia nafasi wanazopata katika mechi zao za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana wakiwa njiani kurejea jijini Dar es Salaam wakitokea Mwanza, Vivier alisema kuna tofauti kubwa kati ya mechi waliyocheza juzi dhidi ya Gwambina FC na mbili zilizopita dhidi ya KMC na Yanga, kwa kuwa wachezaji wao walionyesha hali ya kujituma zaidi.

Alisema ameona mabadiliko hayo kwa wachezaji kujituma na kupambana kupata pointi mbili ugenini (Kanda ya Ziwa), lakini tatizo bado ni umakini kubadilisha nafasi wanazotengeneza kuwa mabao.

"Ni kweli hali ya kujituma imekuwapo kwa hizi mechi mbili, dhidi ya Gwambina tumetoka suluhu na dhidi ya Biashara United mchezo ulimazika kwa sare ya bao 1-1, nimeona kiwango kikubwa, tatizo lipo kwa washambuliaji kumalizia nafasi za mwisho.

"Nafasi ya Dube inaonekana, ila ninaimani Kocha Mkuu, George Lwandamina ameona pakuanzia kufanyia kazi," alisema.

Alisema sasa wanarejea jijini kwa ajili ya kujiandaa na mechi yao dhidi ya Namungo FC, hivyo watapambana kupata matokeo chanya ambayo yatawarejesha katika ari yao ya awali.

Baada ya matokeo hayo, sasa Azam FC imefikisha pointi 27, lakini inaendelea kubaki katika nafasi ya pili wakizidiwa alama saba na vinara, Yanga baada ya timu hizo kila moja kucheza mechi 14, huku mabingwa watetezi, Simba wakishika nafasi ya tatu kwa pointi 23 baada ya kushuka dimbani mara 11.



Mshambuliaji wa Azam FC, Iddi Nado, akipiga hesabu za kumtoka beki wa Gwambina FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyopigwa Uwanja wa Gwambina, Misungwi jijini Mwanza juzi na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

# Lwanga anusa ushindani Simba

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya kukishuhudia kikosi cha timu yake kikilazimishwa suluhu kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Plateau United wiki iliyopita, kiungo mkabaji mpya wa Klabu ya Simba, Mganda Taddeo Lwanga, amesema kuna changamoto kubwa ya kuweza kumshawishi kocha mazoezini ili kuchomoza kikosi cha kwanza.

Licha ya matokeo hayo, Simba imesonga mbele kutokana na ushindi wao wa bao 1-0 walioupata ugenini nchini Nigeria kwenye mechi ya awali, hivyo sasa itakutana na FC Platinum ya Zimbabwe kwenye raundi ya kwanza.

Endapo Simba ambayo inashuka Uwanja wa Benjamini Mkapa leo kuikaribisha Polisi Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, itaitoa FC Platinum, itatinga moja kwa moja hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, michuano ambayo inaongoza kwa utajiri barani humu kwa ngazi ya klabu.

Hata hivyo, mbali na kuishuhudia timu hiyo ikicheza mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Plateau United, pia Lwanga ambaye anasubiri dirisha dogo la usajili Tanzania Bara lifunguliwe hapo Desemba 15, mwaka huu ili kukamilisha taratibu za usajili na kuanza kuitumikia Simba kwenye michuano mbalimbali, tayari ameanza mazoezi na wachezaji wenzake.

Kiungo huyo ambaye amechukua nafasi ya Mbrazil Gerson Fraga, amesema uwezo anaoushuhudia kutoka kwa wachezaji wenzake katika mazoezi unampa changamoto kubwa ya kufanya ili kupata nafasi katika kikosi cha kwanza.

"Katika mechi dhidi ya Plateau United, nimekiona kikosi cha Simba na kuna wachezaji wengi wazuri wenye uzoefu, hivyo kuna kazi ya kufanya ili kuwa bora.

"Kwa ujumla maisha ya hapa ninayafurahia, ninaamini kuwapo kwangu hapa tutashirikiana na wenzangu ili kupata kile ambacho tunakihitaji," alisema straika huyo fundi wa mashuti ya mbali.

Katika raundi hii ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba itaanzia tena ugenini dhidi ya FC Platinum kati ya Desemba 22-23, kabla ya kurudiana Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kati ya Januari 2-3, mwakani.

## Dulla Mbabe sasa ampania Mmalawi

Na Shufaa Lyimo

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini Abdallah Pazi(Dulla Mbabe) ametamba kumpiga mpinzani wake kutoka Malawi, Simon Tcheta, katika pambano la usiku wa mabingwa litakalofanyika Desemba 26, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana na gazeti hili, bondia huyo alisema amejipanga vizuri kutokana na mazoezi anayoendelea kuyafanya.

Dulla Mbabe alisema kwa sasa anataka kuwakata midomo baadhi ya watu ambao wanambeza baada ya kutofanya vizuri alipopigana na Bondia Twaha Kiduku kutoka Morogoro.

"Sasa hivi sitaki dharau nimejipanga kufanya vizuri katika pambano hilo, ninaomba mashabiki wangu wajitokeze kwa wingi siku hiyo," alisema Dulla Mbabe.

Naye Promota wa pambano hilo, Selemani Semunyu, amesema maandalizi yanaendelea vizuri na kuwataka wadau na mashabiki wanunue tiketi mapema.

"Tunaomba Watanzania waje kwa wingi siku ya mapambano tunasisitiza kununua tiketi mapema," alisema Semunyu.

## Gwambina kupotezea usajili wa dirisha dogo

Na Shufaa Lyimo

BENCHI la Ufundi la Klabu ya Gwambina, limesema kwa sasa halifikirii tena kufanya usajili pindi dirisha dogo la usajili Tanzania Bara litakapofunguliwa Desemba 15, mwaka huu kutokana na kuridhishwa na viwango vya wachezaji wao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Fulgence Novatus, alisema wachezaji aliokuwa nao wana uwezo mzuri na wameendelea kuimarika kila uchao.

"Kwa sasa sifikirii suala la usajili kwa kuwa wachezaji ambao ninao wana uwezo mzuri, ila muda ukifika nitajua kama nitasajili au laa," alisema Fulgence.

Kocha huyo alisema mchezo uliopita dhidi ya Azam FC ambao walitoka suluhu, matokeo hayo yalichangiwa na wachezaji wake kutozitumia vizuri nafasi walizotengeneza.

"Tunashukuru tumecheza na timu kubwa japokuwa hatukupata matokeo mazuri tukiwa nyumbani, wachezaji wangu walipata nafasi nyingi isipokuwa walishindwa kuzitumia," alisema.

Alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri wanajiandaa na mchezo ujao dhidi ya Dodoma Jiji FC ambao utapigwa Desemba 13, mwaka huu.

# Michezo

Jumatano Desemba 9, 2020

Nipashe




POGBA MUDA WAKE UTD UMEISHA - RAIOLA HABARI UK 22

WAMEREJEA...



Mastraika wa Simba, Chris Mugalu (kushoto) na Meddie Kagere, waliokosekana kwa muda mrefu kutokana na kuwa majeruhi, ambao sasa wamereja kikosini baada ya kupona, hivyo kumpa uwanja mpana Kocha Mkuu Sven Vandenbroeck wa kupanga kikosi chake kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Polisi Tanzania itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo. **PICHA: MAKTABA**

# SIMBA SASA YAGEUZIA 'PIRA BIRIANI' LIGI KUU

●●●Sven awataka wachezaji kusahau michuano ya CAF na kuokota tatu za Polisi Tanzania leo wakati...

**Na Saada Akida**

HUKU wakitamba na soka lao la pasi sahihi fupifupi ama 'Tiki-Taka', ambalo wamelibatiza kwa jina la 'soka biriani', mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, leo wanarejea dimbani kwenye kinyang'anyiro cha ligi hiyo baada ya wiki iliyopita kufanikiwa kutinga hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba imetinga hatua ya kwanza ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), kwa kuitoa Plateau United ya Nigeria baada ya kushinda bao 1-0 ugenini na kulazimishwa suluhu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, hivyo sasa itakutana na FC Platinum ya Zimbabwe hatua inayofuata.

Hata hivyo, leo inarejea kwenye Ligi Kuu Bara kutetea ubingwa wake kwa kuikaribisha Polisi Tanzania katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa majira ya saa 10:00 alasiri.

Simba ambayo jana na juzi ilikuwa katika mazoezi makali kwenye Uwanja wao wa Simba Mo Arena, uliopo Bunju jijini Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, atakuwa na uwanja mpana wa kupanga safu yake ya ushambuliaji kutokana na nyota wote watatu, John Bocco, Meddie Kagere na Chris Mugalu kuwa tayari kwa mchezo.

**Kuelekea mchezo huo wa leo, Sven amesema wachezaji wote wapo vizuri na tayari kwa ajili ya mechi hiyo kuhakikisha wanapata matokeo chanya.**

Alisema anaamini mechi itakuwa ya ushindani mkubwa na kuwataka wachezaji kusahau michuano ya kimataifa na kuelekeza nguvu zao katika mechi za Ligi Kuu zinazowakabili kwa sasa wakianza na hii ya leo dhidi ya Polisi Tanzania.

"Hakuna kudharau timu, bado tunaendelea kusimama katika mstari tulioanza nao wa kufanya vizuri Ligi ya Mabingwa pamoja na msimu huu kutetea ubingwa wetu, kwa malengo hayo wachezaji wanalazimika kucheza katika hali ya kujituma kutafuta ushindi dhidi ya Polisi leo," alisema Sven.

Alisema anawaheshimu wapinzani wao, hivyo wataingia uwanjani kwa tahadhari kuhakikisha wanapata matokeo chanya katika mechi hiyo ambayo anahitaji pointi tatu muhimu.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale, alisema maandalizi ya timu yake yapo vizuri, na anaamini mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wanakutana na timu kubwa ambayo pia ni mabingwa watetezi.

"Itakuwa mechi ya ushindani mkubwa, tunahitaji kucheza kwa tahadhari kubwa kutafuta pointi muhimu, tunatambua Simba ni mabingwa wanakuja kutafuta ushindi ili kufikia malengo yao ya kutetea taji hilo, lakini pia tunatambua wametoka kufanya vizuri katika mechi za kwanza za michuano ya kimataifa," alisema Malale.

# YANGA YATEUA MAWAKILI KUISUKA

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Klabu ya Yanga, Dk. Mshindo Msolla, kwa kushirikiana na Kamati yake ya Utendaji, wameonyesha hawataki kufanya makosa kuelekea kuingia katika mfumo mpya wa uendeshaji wa klabu hiyo, baada ya kuteua kamati ndogo ya watu makini.

Katika Kamati Ndogo ya Mabadiliko iliyotangazwa jana na Dk. Msolla, ni ya watu wanane, ambayo inajumuisha mawakili watano.

**Kamati hiyo inaongozwa na Mwenyekiti, Wakili Raymond Wawa na Wajumbe; Wakili Sam Mapande, Wakili Audats Kahendagile, Wakili Imani Madega, Wakili Mark Anthony huku wajumbe wengine wakiwa ni Mohammed Msumi, Pastory Kiyombia na Deborah Mkemwa.**

Uteuzi huo wa watu makini kuelekea mchakato huo wa mabadiliko ni mwendelezo wa hatua sahihi zinazochukuliwa na Dk. Msolla kwani katika Kamati Kuu ya Mabadiliko pia inaundwa na wabobezi wa sheria na wasomi mbalimbali.

Kamati Kuu ya Mabadiliko ya Yanga ipo chini ya Mwenyekiti, Wakili Alex Mgongolwa na Wajumbe; Mtaalamu wa Katiba na Sheria za Ardhi, Profesa Mgongo Fimbo, Mkuu wa Mkoa Mstaafu, Said Mecki Sadiki, Mchumi Mohamed Nyenge, George Fumbuka ambaye ni mshauri wa masuala ya uwekezaji na Felix Mlaki - mchumi na mtaalamu wa masuala ya fedha.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002